# Nipashe

Jumamosi Mei 4, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579909

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## JPM amtumbua meneja wa Tanesco kiwandani

UKURASA 4




UKURASA 13

# Mkapa: Dk. Mengi alinifanya Rais bora

UKURASA 2




" Taifa limepoteza mwekezaji mzalendo anayejali wanyonge

**RAIS SHEIN**

" Dk. Mengi alikuwa muumini wa utoaji. Tutamkumbuka pia kwa mchango wake kutunza mazingira.

**SPIKA NDUGAI**





" Dk. Mengi alinifanya kuwa rais bora kwani siku zote alikuwa mkweli na mwenye msimamo thabiti anapotoa maoni yake.

**RAIS MSTAAFU BENJAMIN MKAPA**

" Mzee Mengi hakuwa mbaguzi, aliwatazama watu wa dini nyingine na aliwajali Watanzania wote.

**MUFTI ZUBEIR**





## ... kuzikwa Alhamisi Kilimanjaro

- **Mabalozi**, wakuu wa mikoa wamlilia...*Endelea ukurasa 2&3*

**MICHEZO** IGANGULA KUTIMIZA NDOTO ZA DK. MENGI UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



HUZUNI 1942 - 2019

## Bakwata: Alijali watu wa dini zote

**Na Gwamaka Alipipi**

BARAZA la Waislamu Tanzania (Bakwata), limesema litamkumbuka Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi kwa kuwasaidia katika ujenzi wa misikiti nchini, ukiwamo Msikiti Mkuu wa Muheza pamoja na madrasa mbalimbali.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mufti wa Tanzania, Sheikh Mkuu Abubakar Zubeir Ali, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelezea mwandamo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema Bakwata imepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha Dk. Mengi kwa sababu alikuwa ni msaada mkubwa kwa Waislamu na jamii yote ya Watanzania.

"Mzee Mengi hakuwa mbaguzi, aliwatizama watu wa dini nyingine na aliwajali Watanzania wote, hakika sisi tutamkumbuka kwa namna alivyotusaidia, tumeishi naye katika hali hiyo," alisema Mufti Zubeir.

Alisema Bakwata itamkumbuka Dk. Mengi kwa msaada alioutoa katika ujenzi wa misikiti hapa nchini pamoja na madrasa na kwamba kifo chake kimeacha simanzi kwa Waislamu wote.

Alisema enzi za uhai wake, Dk. Mengi alikuwa akiwajali wagonjwa na maskini na wala hakuwa mtu aliyejikweza na alipenda sana kuwasaidia wasiojiweza na kwamba alikuwa mtu mcheshi.

Mufti Zubeir alisema Dk. Mengi alikuwa mtu aliyekuwa akianzisha mambo na kuyafuatilia na kwamba ndiye aliyekuwa mwasisi wa kwanza wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Dar es Salaam, akishirikiana na Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi.

## Dk. Shein: Mengi atakumbukwa kwa uzalendo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ametuma salamu za rambirambi kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wafanyakazi wa IPP Media kufuatia kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Dk. Reginald Mengi.

Dk. Shein alieleza kuwa amepokea kwa mshtuko na huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Dk. Mengi na kueleza kuwa yeye binafsi pamoja na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania nzima kwa jumla wamejawa na simanzi nzito kufuatia msiba huo mkubwa wa kitaifa.

"Kwa hakika msiba huu umetugusa Watanzania sote, ni msiba wetu kwa sababu aliyefariki ni ndugu yetu, mwenzetu, mfanyabiashara, mwekezaji mzalendo

INAENDELEA UK. 4

# Mkapa: Dk. Mengi alisababis

NIMEPOKEA kwa mshtuko mkubwa na huzuni isiyo na kifani habari za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi.

Nimemfahamu Dk. Mengi kwa miaka mingi sana na kwangu mimi Dk. Mengi ni mzalendo wa kweli ambaye alisimama imara na kujitolea kwaajili ya manufaa ya Watanzania wengi.

Alikuwa miongoni mwa wazawa walioanzisha na kuendesha viwanda ambao sisi serikalini tulijivunia kwa hakika.

Dk. Mengi alikuwa mtu ambaye hakuwa mbinafsi na alipenda sana kuona watu wanaondokana na umaskini.

Dk. Mengi alikerwa sana na tofauti ya kipato miongoni mwa Watanzania hivyo alitumia muda wake mwingi kutatua kero ya umaskini kwenye jamii ya Watanzania. Dk. Mengi alikuwa mtu wa kipekee sana na mzalendo wa kweli aliyefanya mambo mengi mema kwaajili ya taifa lake.

Wakati wa urais wangu hasa wakati wa mikutano na mikusanyiko mbalimbali, Dk. Mengi alinifanya kuwa rais bora kwani siku zote alikuwa mkweli na mwenye msimamo thabiti anapotoa maoni yake hata kama yatatofautiana na msimamo wangu na hali hiyo ndiyo iliniwezesha kunufaika kwani nilichota busara zake.

Wajibu wa Dk. Mengi wa kusaidia kukuza sekta binafsi ni jambo bayana ambalo halihitaji msisitizo mkubwa kwani ni yeye aliyekuwa mstari wa mbele kuipigania na kuikuza.

Katikati ya hayo yote aliyoyafanya, kama tunataka kumuenzi vyema Dk. Mengi njia bora ni kuendelea kuwa wanyenyekevu katika nafasi mbalimbali za uongozi tunazopata katika jamii kwa kufuata nyayo zake katika kusaidia jamii kuondokana na umaskini badala ya kudhani kuwa hilo ni jukumu la serikali pekee.

Tutamkumbuka daima na kumuenzi Dk. Mengi kwa kutambua kuwa kuna vitu vikubwa duniani zaidi ya fedha, umaarufu au madaraka.

Kwa ubora wake, Dk Mengi alituonyesha kwamba vitu vyote hivyo yaani fedha, umaarufu na madaraka haviwezi kuwa juu ya uzalendo, utu na unyenyekevu.

Dk. Mengi umetuachia deni. Mungu aiweke roho yako pahala pema peponi. Amina.

Mwandishi ni Benjamin Mkapa aliyekuwa Rais wa Tanzania 1995-2005.



# Uingereza, Marekani, waku

KAIMU Balozi wa Marekani Tanzania, Dk. Imni Patterson, amesema mchango wa Dk. Reginald Mengi, katika sekta ya habari na taifa kwa ujumla haupimiki.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani, yanayofanyika kitaifa mkoani Dodoma, alisema alijitoa kuendeleza ukuaji wa sekta ya habari na maendeleo yake kwa ujumla.

Alisema Ubalozi wa Marekani umepokea kwa masikitiko makubwa na unatoa pole kwa familia na wana IPP kwa ujumla.

Naye, Balozi wa Uingereza nchini, Sahah Cooke, alisema Dk. Mengi aliibadilisha sekta ya habari na kugusa maisha ya Watanzania wengi kwa namna tofauti.

"Mengi aligusa maisha ya wengi kwa namna tofauti tofauti, alibadilisha sekta ya habari Tanzania, atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa," alisema.

Mkuu wa mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amesema maisha ya Dk.Regnald Mengi ni alama kubwa kwa Watanzania, na kuwa mafanikio yake ya biashara yaliwapa watanzania wengi fursa za ajira, ubunifu na mtaji.

Pia simulizi ya historia ya maisha yake ilijenga uthubutu kwa wengi.



Dk. Faustine Ndugulile



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira

"Mzee Mengi alikuwa mtu wa kusikiliza, alijitoa kwa sana katika elimu (Maasai Girls na kwingineko), kampeni za afya, michezo, kuwakarimu wenye ulemavu, kuwatia moyo wajasiriamali wadogo (vicoba) na mambo ya dini na bado ulisimama kama taswira ya mfanyabiashara mtanzania aliyeheshimika kitaifa na kimataifa,"ameeleza Mtaka.

Pi alimuelezea Dk. Mengi kuwa hata faida aliyoipata katika biashara zake alirejesha sehemu kwa watanzania waliopata matatizo, magonjwa ya moyo na kansa.

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amemuelezea Dk. Mengi kama mtu muhimu ambaye mkoa wa Kilimanjaro hau-



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka

HUZUNI 1942 - 2019

# sha nikawa Rais bora



Michael Ngalo, msemaji wa familia ya Mwenyekiti Mtendaji wa IPP Ltd, marehemu Dk. Reginald Mengi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# u wa mikoa wanena



Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini, Inmi Patterson



Balozi wa Uingereza hapa nchini, Sarah Cooke.

wezi kumsahau kwa mchango wake katika uchumi na nyanja nyingine ikiwamo sekta ya viwanda na kilimo.

"Kifo chake ni zaidi ya pigo kwa maendeleo na hasa katika mkoa wa Kilimanjaro. Hapa Kilimanjaro alikuwa anatutia moyo akisikia tumefanya jambo jema na alikuwa anaongeza na mawazo yake. Naamini watoto wake watayaendeleza yale aliyokuwa akiyafanya wakati ule akiwa hai, kwani ndio sehemu ya mafanikio yake," alisema.

Naibu Waziri wa Afya Dk. Faustine Ndugulile, alisema, amepokea kifo cha Dk. Mengi kwa masikitiko makubwa kwa sababu hivi karibuni walikutana na kuongea kuhusu uanzishaji wa huduma ya 'stem cell therapy' nchini.

**Imeandikwa na Salome Kitomari na Geofrey Mushi (Dodoma)**

# ...Kuzikwa Alhamisi mkoani Kilimanjaro

**Waandishi Wetu**

MWILI wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, unatarajiwa kuwasili nchini keshokutwa kwa ndege ya Shirika la Emirates ukitokea Dubai, Falme za Kiarabu.

Msemaji wa familia, Michael Ngalo, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akitoa ratiba nzima ya shughuli ya mazishi ya mwili wa mfanyabiashara huyo aliyefariki dunia usiku wa kuamkia juzi nchini humo.

Alisema mwili huo baada ya kuwasili nchini, utapelekwa Hospitali ya Jeshi Lugalo na Jumanne utapelekwa Viwanja vya Karimjee ili kuagwa.

"Jumanne asubuhi, mwili utaondolewa Lugalo na kupelekwa Viwanja vya Karimjee kwa ajili ya kuagwa na baadaye utarudishwa nyumbani kwake Kinondoni kwa maombi na Jumatano asubuhi, mwili utapelekwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kwa ajili ya kusafirishwa kwenda Moshi mkoani Kilimanjaro na kupelekwa moja kwa moja Machame na utalala hadi asubuhi," alisema.

Ngalo aliongeza kuwa ibada ya mazishi itafanyika Alhamisi katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Kiseren na baadaye utarudishwa nyumbani kwa ajili ya mazishi.

**SALAMU MSIBANI**

Akiwa msibani nyumbani kwa marehemu jijini Dar es Salaam jana, Mbunge wa Vunjo, James Mbatia, alizungumza na waandishi wa habari na kueleza kuwa Dk. Mengi alipenda kusema 'kubali ukweli ulivyo na uweze ukaendana nao'.

"Ili kuweza kuchukua yote mazuri aliyoyafanya Dk. Mengi, siyo kwa Watanzania tu, kwa dunia, basi tuyachukue matendo yake mema yaliyo mengi kama jina lake,

INAENDELEA UK. 8

# Spika Ndugai amwita Mengi 'Philanthropist'

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai jana, 'alichora' picha ya mtu mzalendo na mwenye huruma kwa maskini na wanyonge katika siku zote za maisha yake ya kila siku wakati wa uhai wake duniani, alipotoa salamu za rambirambi za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk.Regnad Mengi.

Akitoa salaam hizo kabla ya kuanza kwa shughuli za Bunge, Spika Ndugai alisema Dk. Mengi alijulikana zaidi kwa Watanzania kwa utoaji wake wa misaada ya kijamii, akisema alikuwa 'Philanthropist' (muumini mkubwa wa utoaji wa misaada).

Amemuelezea katika uhai wake kuwa Dk. Mengi alijitoa hasa katika ujenzi wa misikiti, makanisa na alijitoa sana kwa maskini na watu wasiojiweza,wanyonge, walemavu na alisaidia sana katika maeneo ya tiba kwa wagonjwa wakiwamo wa moyo.

Spika Ndugai katika salaam zake alisema Dk. Mengi atakumbukwa katika siku za usoni kwa kuchangia Sh. milioni 50 kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwaunga mkono kwenye mradi uliobuniwa na Wabunge Wanawake (TWPG) wa kujenga vyoo vya mfano kwa mtoto wa kike katika majimbo yote Tanzania.

"Dk. Mengi alikuwa ni Mtanzania ambaye kwa bidii, juhudi na maarifa aliweza kukua kiuchumi kutoka maisha duni ya kijijini hadi kufikia kuwa mmoja wa wafanyabiashara wakubwa hapa kwetu Tanzania, Afrika Mashariki na Duniani kwa ujumla," alisema na kuongeza:

"Katika kuomboleza kifo na msiba huu mkubwa, sisi Bunge tunaungana na Mheshimiwa Rais, Dk. John Magufuli, familia ya marehemu na Watanzania wote, tukimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa mchango wake mkubwa usiopimika kwetu Watanzania.

Tutamkumbuka daima sisi kwa jinsi ambavyo alisaidia sana hifadhi ya mazingira hasa maeneo yanayozunguka Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro kwa kupanda miti mingi sana kwa mamilioni bila kuchoka."

Aidha, Spika Ndugai alimuelezea Dk. Mengi licha ya kuwa mmiliki wa vyombo mbalimbali vya habari, alikuwa mmiliki wa viwanda kadhaa hasa katika sekta ya uzalishaji.

Pamoja na mambo mengine aliyoyafanya wakati wa uhai wake, Spika Ndugai ameeleza kuwa Dk. Mengi alikuwa kiongozi wa umma akiwa ni Mwenyekiti wa bodi mbalimbali ikiwamo IPP na nyingine nyingi za binafsi na umma.

## Dk. Shein: Mengi atakumbukwa

INATOKA UK. 2

na aliyekuwa akiwajali wanyonge wakiwamo wananchi wa rika zote pamoja na watu wenye ulemavu, wanamichezo na wapenda mazingira," ilieleza sehemu ya salamu za rambirambi za Dk. Shein.

Aidha, Rais Shein alisema kuwa kwa vile kifo ndio mwisho wa uhai wa mwanadamu, alimuomba Mwenyezi Mungu aijaalie roho ya marehemu Dk. Mengi alilaze mahala salama.

Dk. Shein alieleza kuwa wananchi wa Zanzibar wanaungana na ndugu, jamaa, wafanyakazi wa IPP Media na marafiki wa marehemu katika msiba huo mzito.

Dk. Shein alimuomba Mwenyezi Mungu awape Watanzania wote na wanafamilia nyoyo za subira katika kipindi hiki kigumu cha msiba.

Katika salamu hizo, Dk. Shein alieleza kuwa hatomsahau marehemu Dk. Mengi kwa juhudi zake kubwa katika suala la uhifadhi wa mazingira ambaye aliweza kushirikiana naye kwa kiasi kikubwa wakati Rais Dk. Shein akiwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Dk. Mengi akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC).

Dk. Shein alieleza kuwa marehemu Dk. Mengi ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), , alihamasisha Maendeleo ya Kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kwa kuchangia ukuaji wa sekta binafsi kuendana na soko la pamoja kwa nchi wanachama.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa, bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: OWM

# JPM amtumbua meneja wa Tanesco kiwandani

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli, amemtumbua Meneja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), Mkoa wa Mbeya, kwa kushindwa kufika kwenye hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanda cha Saruji cha Mbeya.

Rais Magufuli alimwagiza Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, kumhamisha mtendaji huyo kwa kushindwa kufika eneo hilo.

Aliagiza meneja huyo ambaye amefanya kazi katika Mkoa huo kwa miaka minne, atolewe arudishwe alikotoka na apangwe mtumishi mwingine atakayeshughulika na masuala ya umeme.

"Yuko wapi huyo Meneja wa Tanesco, angekuwa hapa si angejibu maswali, Waziri Lukuvi mpigie simu Kalemani, ateue Meneja mwingine wa Tanesco Mbeya kuanzia kesho (leo) aje aanze kazi mara moja," alisema Rais Magufuli.

Alihoji sababu za meneja huyo kulala nyumbani ilihali mameneja wengine wa idara tofauti katika mkoa huo, walikuwa wamefika katika ziara yake hiyo.

"Mpaka meneja wa Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) yupo hapa nikimsimamisha kazi hapa nitakuwa nimefanya kosa? Wangapi wanakubaliana na mimi, safi kabisa, kuanzia leo yeye 'out' akajifunze vizuri kutafuta umeme hatufai tena hapa Mbeya," Rais Magufuli alisema.

Pia Rais Magufuli aliahidi kufanyia kazi changamoto ya kukatika umeme katika kiwanda hicho linalosababisha hasara kwamba serikali italifanyia kazi.

**AITEGA TBA**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli ameutaka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), kuboresha utendaji kazi wao na endapo wataendelea kuwa wazembe taasisi za umma ziwanyime zabuni za ujenzi.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana jijini Mbeya wakati akiweka jiwe la msingi katika upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (Must) ikiwa ni siku yake ya tisa ya ziara zake mkoani humo.

INAENDELEA UK. 8

# Ghasia aipa kibano serikali maji

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Mtwara Vijijini CCM), Hawa Ghasia, ameendelea kuwa mwiba mkali kwa serikali, baada ya kudai ndani ya Bunge anaona giza nene katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara Mjini ambao Waziri wa Maji na watendaji wake wameutengea fedha lakini hawajui kama upo.

"Mradi ule ukitekelezwa utapeleka maji katika vijiji vya Mtwara Vijijini zaidi ya 30, lakini mpaka sasa hivi huu mradi umekuwa ukisuasua na ukikutana na watendaji wanakwambia mradi upo na wakati mwingine ukikutana na Waziri anasema huu mradi haupo,"alisema

Ghasia aliyewahi kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) wakati wa utawala wa awamu ya nne na baadae kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Bunge la 11, alisema ana wasiwasi kwa sababu baada ya kupitia bajeti amekuta sehemu umeandikwa mradi huo umetengewa Sh. bilioni moja.

"Waziri atakapokuja kutoa majibu atuambie mradi huu wa maji katika mto Ruvuma upo au haupo? na kama haupo sisi wa Mtwara Vijijini vile vijiji ambavyo vilipangiwa kupata maji katika mradi huu vitapelekewa maji kwa mradi gani.

INAENDELEA UK. 8



# HUZUNI 1942 - 2019



Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Lazaro Mambosasa, akisaini kitabu cha maombolezo alipofika kuhani msiba wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, nyumbani kwa marehemu, Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mama Anne Kilango Malecela ambaye ni Mke wa Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela (aliyesimama), akisaini kitabu cha maombolezo nyumbani kwa marehemu. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Baadhi ya maofisa waandamizi wa polisi waliofika kuhani msiba nyumbani kwa marehemu. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Baadhi ya waombolezaji wakiwasili msibani. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi na Mbunge wa Vunjo, James Mbatia (kushoto), akibadilishana mawazo na Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, walipokutana msibani. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko (wa pili kulia), akiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, na baadhi ya viongozi wa klabu ya waandishi wa habari, mkoani Shinyanga, wakiwa wamesimama kwa dakika moja, kufuatia kifo cha Mwenyekiti Mtendaji IPP, Dk. Reginald Mengi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Habari, wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Wanamichezo waeleza kuwa bado walimhitaji Dk. Mengi*

**WAKATI** taarifa kutoka katika familia ikisema kuwa mwili wa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, unatarajia kuwasili nchini Jumatatu ukitokea Umoja wa Falme za Kiarabu, bado salamu za pole zimeendelea kutolewa kutoka kwa wanamichezo mbalimbali wa hapa nchini.

Marehemu Dk. Mengi ambaye alionekana wazi zaidi akishiriki katika kusaidia maendeleo ya mpira wa miguu nchini kupitia timu za Taifa (Taifa Stars na Serengeti Boys), pia alikuwa akisaidia michezo mingine kwa namna mbalimbali.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema katika taarifa yake kuwa bado nchi ilikuwa inahitaji zaidi mchango wake katika kufikia malengo ya kufanya vema katika mashindano mbalimbali. Karia alisema kuwa mfanyabiashara huyo alikuwa ni kiongozi ambaye hataki kuona timu inataka tamaa hapa pale ilipobainika kwamba hakuna nafasi ya kufanya vizuri. Alisema kuwa hilo peke yake lilionyesha wazi mapenzi yake kwa nchi na kila siku alikuwa ni mtu mwenye kuamini Tanzania itaweza kufanya vema na kusahau maumivu ya kuvurunda yaliyokuwa yanazizunguka timu za hapa nchini kila zilizoshiriki mashindano ya kimataifa.

Alieleza kwamba tangu alipotangazwa kuwa mlezi wa Timu ya Taifa ya Vijana wa umri chini ya miaka 17 maarufu Serengeti Boys, alitaka kujua maendeleo ya kikosi hicho na programu zake ili kuwapa chipukizi hao mazoezi ya kutoka kuelekea Fainali za Vijana za Afrika (AFCON U-17) ambazo zilimalizika hivi karibuni kwa Cameroon kutwaa ubingwa.

Licha ya Serengeti Boys ambao walikuwa wenyeji wa fainali hizo kufanya vibaya kuanzia katika mchezo wa ufunguzi dhidi ya yosso wenzao kutoka Nigeria kwa kufungwa mabao 5-4, marehemu Dk. Mengi aliwataka Watanzania kuendelea kuishangilia timu hiyo akiamini ndio kwanza safari ya mafanikio imeanza.

Kauli mbiu yake maarufu ya I can, I Must, I Will pia ilikuwa ni sehemu ya maneno ya kila siku ya wachezaji wa Serengeti Boys tangu walipokuwa wanacheza mechi za maandalizi kuelekea fainali hizo.Alifanikiwa kuwajenga ujasiri yosso hao na hii iliwasaidia kufanya vema wakati wa maandalizi kwa kubeba makombe mbalimbali na kuonekana kuwa ni moja ya timu tishio.

Ukiondoa ushiriki wake huo katika soka la vijana, marehemu Dk. Mengi alishiriki kikamilifu kuiongoza Kamati ya Ushindi ya Taifa Stars wakati ikisaka tiketi ya kucheza Fainali za Afrika za mwaka 1994. Chini ya uongozi wake, Taifa Stars ilifanya vema kwa kushinda mechi zake zote za nyumbani ilipocheza dhidi ya Algeria, Sudan na Uganda, lakini iliteleza kwenye michezo ya ugenini.


Pia katika kuhakikisha anapenda maendeleo, alikuwa katika mstari wa mbele kutatua mgogoro uliokuwa unawatafuna vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao uliwagawa katika makundi mawili yaliyojulikana kwa jina la Yanga Asili na Yanga Kampuni. Aliwataka wanachama wa Yanga kukubaliana na mazingira halisi akiamini kwamba mabadiliko ya mfumo ndiyo suluhisho pekee litakalowaondoa kwenye hali ya utegemezi, jambo ambalo sasa miaka 25 limepita na wanachama hao wanalidai.

Kama mzalenzo, aliwapa nafasi Watanzania wenzake mwaka 1994, kushuhudia fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa kuweka "screen" kubwa katika maeneo mbalimbali bila ya gharama zozote, hasa ikizingatiwa miaka hiyo idadi kubwa ya familia zilikuwa hazina televisheni. Pia mafanyabiashara huyo aliwapa burudani nyingine wadau wa soka nchini kwa kushuhudia fainali za Kombe la Dunia mwaka huo huo kupitia kituo chake cha televisheni cha ITV bila malipo yoyote, tofauti na ambavyo sasa makampuni yanayomiliki ving'amuzi yanavyoshindana kujitangaza.

Mungu aipumzishe roho ya Dk. Mengi mahali pema peponi. **Amen.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## *Mengi, mbele yetu nyuma yako*

Na Barnabas Maro

**NI** vigumu kukumbuka mambo mengi aliyofanya Dk. Reginald Mengi wakati wa uhai wake. Kwa hakika ni mengi kama lilivyo jina lake.

Kama kumbukumbu zangu ni sahihi, nilianza kufahamiana na Dk. Mengi mwanzoni mwa miaka ya 80 wakati ule nikiwa Mhariri wa Habari wa gazeti la Kiongozi linalochapishwa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC). Wakati ule pia nilikuwa mmoja wa viongozi wa Chama cha Waandishi wa habari nchini. Tulikutana na Dk.Reginald Mengi mara kwa mara kila viongozi wa chama cha waandishi wa habari tulipokutana. Nakumbuka wakati fulani tukiwa tunakula chakula cha mchana alichotuandalia kwenye hoteli maarufu ya jijini Dar es Salaam alituuliza kama tumesikia tetesi kuwa ameombwa awe na hisa katika gazeti la Kiingereza liitwalo Business Times.

Wakati tukiendelea kumsikiliza, akasema kamwe hawezi kuchukua hisa kwenye vyombo vya habari, hasa magazeti. "Ukitaka kugombana na serikali, basi kuwa mmiliki wa gazeti... utakuwa na mivutano ya mara kwa mara na serikali," alisema Mengi. Wakati ule alikuwa na biashara yake ya kalamu pembezoni mwa barabara ya Pugu Road ambayo sasa yaitwa Barabara ya Nyerere.

Yaelekea Mengi hakukatishwa tamaa na jambo lolote hasa lililohusu maendeleo yake na ya wengine. Alianzisha kituo cha televisheni (runinga) cha ITV kisha magazeti ya kila siku ya Nipashe (Kiswahili) na The Guardian (Kiingereza) na baadaye magazeti ya mchana na ya kila wiki ambayo aliyasimamisha baadaye.

Nilipostaafu kuwa Mhariri wa gazeti la Mwanachi lililomilikiwa na mhindi ambaye sasa anaishi Canada, Dk. Mengi aliniita kusaidia kazi katika gazeti lake la Nipashe. Nilifanya pale kwa muda wa takriban miaka miwili alipotaka kununua jina la Mwananchi ambalo wakati ule lilikwisha simamishwa. Alinituma nimwombe aliyekuwa mmiliki wa gazeti hilo ili anunue jina na alikubaliwa ingawa hakufanya hivyo.

Baada ya hapo alikuwa na mpango wa kuanzisha gazeti ambalo lingesomeka Kenya, Uganda na Tanzania kama gazeti la nchi moja. Ingawa ilifanyika mipango mingi, mwishowe niliondoka na mpango wa kufungua gazeti hilo ukaishia hewani. Mengi alikuwa mtu mwenye kuona mbele katika biashara zake. Alipoona biashara fulani inampotezea muda na kumwingizia hasara, aliiacha mara. Hakuishia hapo kwenye biashara kwani alikuwa na kiwanda cha kutengenezea chupa za chai lakini akaachana nayo baada ya kutapeliwa kwa kuletewa vifaa bandia vya kutengenezea chupa za chai pale kilipo kiwanda cha Coca Cola jijini Dar es Salaam sasa.

Mengi pia alikuwa na kiwanda cha sabuni za Revola, dawa ya meno (Colgate) na karatasi za chooni. Aliachana na biashara zote alipoona hazimletei faida. Akajikita zaidi katika vyombo vya habari mpaka alipofikwa na mauti kule Dubai.

Kwa jumla ni mtu aliyejali zaidi maendeleo ya jamii na kuwapenda sana walemavu na kuwapa mikopo ya kufungua biashara mbalimbali. Tangu hapo alikuwa na tabia ya kuwaandalia chakula cha mchana kila mwaka na kujadiliana nao kuhusu jinsi ya kupambana na matatizo wanayokumbana nayo.

Nadhani wanamichezo wengi wameguswa na kusikitishwa na kifo cha Dk. Mengi kwani alikuwa mpenzi mkubwa wa michezo akionyesha wazi kuguswa zaidi na klabu ya Yanga. Kuna wakati alimweka mtaalamu wake mkuu wa uchumi kwenye klabu ya Yanga akitaka kuifanya Yanga iongozwe kisasa lakini kwa uroho wa baadhi ya viongozi hawakupenda mpango wake wakijua kama ungekubalika, basi wangekosa fursa ya kula hela za klabu.

Alipoona jitihada zake za kutaka kuifanya Yanga kuwa klabu inayojitegemea yenyewe zinapigwa vita na wasiopenda maendeleo, akaamua kujiweka kando. Bado alikuwa msaidizi mkubwa wa fedha kwa klabu za kandanda kama Taifa Stars, Serengeti Boys bila kuisahau Yanga. Nadhani Yanga watakuwa wakilia chini chini kwani hivi karibuni walipokosa nauli ya kuwapeleka kwenye mchezo fulani, waliienda kumwomba Mengi aliyewawezesha kuendelea na safari yao.

Yanga ingekuwaje leo kama wanachama wangekubaliana na mpango wa Mengi wa kuifanya ijitegemee yenyewe badala ya kuwategemea watu binafsi na kuwa ombaomba?

Mengi alikuwa mtu wa kwanza kuanzisha kampeni ya kupanda miti mkoani Kilimanjaro na kweli miti iliyoonekana kupotea sehemu nyingi za mkoa huo ilirejeshwa kwa juhudi za Mengi aliyetoa zawadi kwa watu waliofanikiwa kupanda miti mingi.

Kwa bidii zake, Mengi alikuwa mwafrika wa kwanza kuanzisha biashara ya maji ya chupa yaitwayo Kilimanjaro yanayouzwa ndani na nje ya Tanzania kupitia kampuni ya Bonite iliyo katika kundi la makampuni ya IPP.

Pamoja na juhudi hizo, pia alikwisha tia saini ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza gesi itakayotumiwa na magari badala ya petroli kule Rwanda. Pia ameacha ujenzi wa viwanda vya madawa humu nchini akishirikiana na wawekezaji wa nje.

Tangulia Mengi tuko nyuma yako. Pumzika kwa amani.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Karibu Tanzania (KTO), Aidan Mchawe (kushoto), akifungua mafunzo kwa walimu wa shule za msingi nchini ya kufundisha wanafunzi kwa vitendo, yaliyofanyika, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ujerumani yatoa bil. 446/- mabadiliko tabianchi Simiyu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na Serikali ya Tanzania zimesaini mkataba wa Euro milioni 171 (sawa na Sh. bilioni 446) kwaajili ya mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi mkoani Simiyu.

Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo iliyosaini mkataba huo ambao mradi wake utawezesha wananchi wa eneo hilo kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwawezesha upatikanaji wa maji endelevu, utunzaji wa mazingira na kilimo kinachovumilia ukame.

Taarifa ya pamoja ya KfW na Ubalozi wa Ujerumani iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, ilieleza kuwa mradi huo utafadhiliwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Ujerumani na Mfuko wa Mapinduzi ya Kijani (GCF), kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani na kutekelezwa na Wizara ya Maji.

Mradi huo unaelekezwa Mkoa wa Simiyu, ambako mvua zake hazitabiriki huku ukame na mafuriko vikitokea mara kwa mara.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mradi huo una lengo la kuboresha maisha ya watu wa eneo hilo kwa kuwaelimisha maeneo yaliyoathirika zaidi na mabadiliko ya tabianchi kwa kusambaziwa majisafi ya kunywa, utunzaji wa mazingira na kilimo.

Mpaka sasa, usambazaji wa maji umekuwa na changamoto kwenye mkoa huo, ambako asilimia 20 pekee ya watu wanaoishi mijini na asilimia 40 ya watu wanaoishi vijijini ndiyo wanaopata majisafi ya kunywa kutoka

**INAENDELEA UK. 8**

# Msimu mpya wa pamba wazinduliwa

**Na Anthony Gervas,**
MWANZA

BODI ya Pamba Tanzania (TCB), imetangaza kufungua msimu mpya wa ununuzi wa zao la pamba, msimu wa 2018/2019 ulianza Mei 2, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi hiyo, Marco Mtunga, alisema kuwa msimu huo wa ununuzi wa pamba umeanza mapema kutokana na mabadiliko ya mfumo mpya wa kilimo cha zao hilo.

"Mabadiliko ya mfumo mpya wa kilimo cha pamba, kila mwaka mkutano mkuu wa Bodi ya pamba utakuwa unafanyika mara mbili kwa mwaka, mwezi Machi na Agosti badala ya Aprili na Novemba...mfumo huo ni wa kilimo chenye kuongeza tija kwa wakulima wa pamba, alisema Mtunga.

Pamoja na kufunguliwa kwa msimu huo mapema, lakini Bodi inaendelea na mchakato wa kutangaza bei elekezi ya wakulima kuuzia, na kuwa msimu uliopita 2017/2018, wakulima waliuza kwa Sh. 1,100 kwa kilo moja ya pamba.

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia kuongeza uzalishaji zaidi wa zao hilo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na Serikali katika kilimo hicho kutokana na wakulima ambao wengi wamekuwa wakilima bila kuzingatia kanuni za kilimo bora kwa kuchanganya mashamba ya pamba na mazao mengine.

Aidha, alisema kuwa wakulima wanahitaji kupewa elimu zaidi juu ya kilimo bora ikiwamo kuzingatia taratibu na kulima kilimo kisasa kitakachowainua kiuchumi.

Alisema pamoja na zao hilo kufufuliwa kwa kasi na Serikali, lakini bado uzalishaji wake uko chini, hivyo bodi itahakikisha yanakuwapo mapinduzi ya kilimo hicho pamoja na ushindani katika mikoa yote inayolima pamba.

Zao hilo ni miongoni mwa mazao matano ambayo serikali imeyaita ya kimkakati. Mengine ni korosho, chai, kahawa na tumbaku.

# Wafanyakazi Bandari kizimbani tuhuma utakatishaji mamilioni

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI wanne wa jijini Dar es Salaam wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na mashtaka manne ya uhujumu uchumi ikiwamo la kutakatisha Sh.milioni 83.

Washitakiwa hao ni Omary Guya (27) Mkazi wa Kigamboni, Godlisten Sammast (33) mkazi wa Kibamba, Froliana Kagisa (27) mkazi wa Buza na Justine Bukuku (28) mkazi wa Buza Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kati ya Machi 2019 na Aprili 6, mwaka huu jijini Dar es Salaam walikula njama ya kutenda kosa la wizi.

Ilidaiwa katika tarehe za tukio la kwanza katika yadi ijulikanayo kwa jina la Uganda iliyopo bandari ya Dar es Salaam, waliiba gari aina ya Toyota VXR-V8 yenye thamani ya Sh. milioni 404,769,692 mali ya Kampuni ya Toyota Tanzania.

Katika shtaka lingine, wanadaiwa washtakiwa hao kati ya Aprili 11 na 12 mwaka huu, wakiwa na nia ya kudanganya walijipatia Sh. milioni 83 kutoka kwa Godfrey Kundi wakidai kwamba wamiliki wa gari hilo, huku wakijua si kweli.

Washitakiwa hao pia wanadaiwa kuwa katika mahali tofauti jijini Dar es Salaam walitakatisha gari hilo kwa kuliuza kwa Sh. miolini 83, huku wakijua gari hilo limetokana na kosa la wizi.

Hakimu alisema washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi, huvyo hawatakiwi kujibu chochote hadi mahakama hiyo itakapopata kibali kutoka kwa Mkurugezni wa Mashitaka (DPP).

"Katika kesi hii pia mnakabiliwa na kutakatisha fedha shtaka hilo halina dhamana," alisema hakimu Kasonde. Alisema washtakiwa wapelekwe mahabusu na kesi itatajwa Mei 17, mwaka huu. Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

**(NBAA)**
**BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU TANZANIA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**SALAMU ZA POLE KUFUATIA KIFO CHA CPA. DKT.REGINALD ABRAHAM MENGI**

**MEI 3, 2019**



Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha CPA. Dkt. Reginald Abrahamu Mengi aliyekuwa mwanzilishi, mmiliki na Mwenyekiti Mtendaji wa Makampuni ya IPP Limited na Mwenyekiti wa nne wa Bodi ya Wakurugenzi wa NBAA (1985-2000).

CPA. Dkt. Reginald Abrahamu Mengi, atakumbukwa kwa uwezo na mchango wake mkubwa katika kuendeleza Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi nchini.

NBAA ilimtumia sana kama mtaalam na mshauri katika kuendeleza taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi nchini na hakika alikuwa mstari wa mbele katika kuendeleza Taaluma hii.

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti, Wafanyakazi na Wanachama wote wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Tanzania tunatoa salamu za pole kwa familia ya Marehemu, ndugu, jamaa na marafiki wote walioguswa na msiba huu.

***BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA, JINA LAKE LIHIMIDIWE***

**Imetolewa na,**
**CPA Pius A. Maneno**
**MKURUGENZI MTENDAJI**

215211302

# ...Kuzikwa Alhamisi mkoani Kilimanjaro

INATOKA UK. 3

tuweze kuyaishi," alisema.

Mbunge huyo alibainisha kuwa Machi 20, mwaka huu, wakati akifanya mazungumzo na Dk. Mengi, aliambiwa na mfanyabiashara huyo kuwa "maisha yapo kwenye ulimi, ukichunga ulimi wako na ukautumia vizuri, utakuwezesha kujenga utu wa mwanadamu na kuheshimu binadamu wenzako".

Mbunge huyo alisema Dk. Mengi alifikia maisha aliyofikia kwa sababu ya kuchunga ulimi wake.

Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, aliwataka Watanzania wamkumbuke Dk. Mengi na kumuenzi kwa yale aliyoyafanya.

Malecela alisema Dk. Mengi ameacha msemo wa mwanafalsafa kutoka Morocco aliyesema "tutakapokuwa tumekufa na tumezikwa kwenye makaburi, msitutafute katika makaburi yaliyopakwa chokaa, ila mtutafute katika mioyo ya wale tuliowahudumia."

Alisema ana uhakika Dk. Mengi ataendelea kuwa kwenye mioyo ya Watanzania.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, alisema wamempoteza mwenzao ambaye kwake ni rafiki.

"Ametuachia mipango mizuri, nitataja mitatu, mtu mwenye utu, alikuwa Dk. Mengi, alikuwa mtu wa kawaida mwenye utu siyo watu wengi wenye utu, alipenda watu wote bila ubaguzi, aliwasaidia bila ubaguzi, aligawa kile alichopata kwa jasho lake, aliamini Mungu ampempa hivyo, akatoa kwa wengine," alisema.

Butiku alisema Dk. Mengi alipenda taifa lake na watu wake na alikuwa mwaminifu na alifanya kazi kwa bidii.

"Alianza na mtaji mdogo, akaukuza na matokeo tumeyaona, alikuwa kijana mdogo, vijana mjifunze kwa mzee huyu aliyetutoka," alisema.

Mbunge wa Kuteuliwa, Anne Kilango, alisema alipokuwa Mbunge wa Same Mashariki, Dk. Mengi alimsaidia kujenga visima vingi.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alisema mkoa wake unaungana na wanafamilia kumuaga Dk. Mengi.

Alisema mfanyabiashara huyo alikuwa mtu mwema na maisha yake yamewafundisha wema na kujifunza duniani wanapita hivyo wasameheane.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, alisema alimfahamu Dk. Mengi kama kiongozi, rafiki na mtu aliyependa watu.

"Nakumbuka nikiwa mbunge niliongoza Watanzania kupambana na ufisadi na Dk. Mengi kupitia vyombo vyake vya habari alipambana na ufisadi, amekuwa msaidizi wa karibu kwa watu maskini, wakati na matajiri pia, amekuwa mfano kwenye mapinduzi ya viwanda.

"Katika kipindi hiki ambacho Rais John Magufuli anajenga Tanzania ya viwanda, nani mwingine atakuwa sauti ya wanyonge? Nani mwingine atakuwa kama yeye? Namna bora ya kumuenzi ni kuyaasisi aliyoamini na kuyasimamia," alisema.

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Enock Charles**

# Ghasia aipa kibano serikali maji

INATOKA UK. 4

"Hivi kweli unaweza ukatoa maji mto Ruvuma ukafikisha Mtwara Mjini kwa Sh. bilioni moja au mheshimiwa Waziri hii ni tocken tu, je utakuwepo? mtaongezea fedha au bado mpo katika kusuasua uwepo au usiwepo? ukija Waziri utupe ufafanuzi."

Mbunge wa Bunda (Chadema), Esther Bulaya, alionyesha kutoridhishwa kwake na Wizara hiyo kutengewa pesa kidogo kwa asilimia 18 hadi asilimia 19.

"Leo bajeti iliyopita tumetenga bilioni 700 imepata bilioni 300. Hivi hizi zilizobaki zinafidiwa lini? na leo wanakuja tena kuomba bilioni 600, ni lazima Bunge tutimize wajibu wetu wa kuibana serikali, unless otherwise (vinginevyo) tutakuwa tunamshambulia Mbarawa wakati serikali haitimizi wajibu wake wa kupeleka pesa za kutosha katika wizara ya maji na maji hayana mbadala," alieleza Bulaya.

Alitaka wabunge kutimiza wajibu wao wa kuibana serikali kama pesa haziendi kama kweli wanataka kuhakikisha pesa zinaenda na kama dhamira yao ya kumkomboa mama na ndoo kichwani wanataka iwe ya kweli.

Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema baada ya bunge kupitisha mabadiliko ya Sheria namba 5 ya inayotoa nafasi ya kuanzishwa kwa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), wakati umefika sasa kwa serikali kufanya maandalizi ya kutosha ili itakapoanza kutekeleza majukumu yake ifanye kazi zake kwa ufanisi.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma (CCM), alishauri upembuzi yakinifu kufanyika ili mradi wa maji unaotarajiwa kuepelekwa eneo hilo utumike vizuri.

Alisema wizara nyingine zinafanya kazi vizuri, lakini changamoto kubwa ipo kwenye wizara ya maji na kuhoji kuna mchawi gani.

"Waziri lazima tukueleze ukweli, Rais anapozunguka kila siku anakueleza kuna wezi ushughuliki nao, anakueleza wizara imeoza hushughuliki nao, Wabunge huku mnamsikia ndugu yangu Kessy (Ally Mbunge wa Nkasi) juzi amesema kuna mwizi kaiba, haushughuliki nao, kwa mawazo yangu natoa ushauri kuwa hata kama tungeongeza shilingi 200, hii Wizara ina wezi zitaenda kuliwa,"

Aliongeza: "Kila Mbunge akisimamishwa ana mradi wa maji lakini umepigwa huku akisema haiwezekani fedha ziongezwe halafu ziliwe hivyo kumtaka Mbarawa afukuze wezi."


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 02/05/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 06/05/2019** kampuni ya **S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR kuelekea KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili: **T776 CAD /T 220 DCT**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18.50** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.00** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

3. NJia itakayotumika DAR hadi **KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215211002



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 02/05/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 06/05/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR kuelekea KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili: **T785 CAD /T 166 ADN .**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **21.80** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.24** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.20** |

3 .NJia itakayotumika **DAR hadi KAGERA kupitia MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215211402


## JPM amtumbua meneja

INATOKA UK. 4

"Natoa wito tena kwa mara ya pili kwa TBA waanze kujipanga, wasipofanya vizuri hata kama ni chombo cha serikali msiwape kazi," alisema Rais Magufuli

Alisema TBA ina wajibu wa kutekeleza majukumu yao kwa wakati katika kazi wanazopatiwa ili kuwahisha miradi ya maendeleo.

"Kwanini mlihangaika kutafuta mkandarasi wa kufanya upembuzi yakinifu na kujenga maktaba wakati kuna wataalam wanafunzi ambao wangefanya kazi ya usanifu? Matokeo yake wamemtafuta mkandarasi aliyewachelewesha kwa miaka saba," alisema Rais Magufuli.

Rais Maguli alihoji sababu ya kuendelea kuikumbatia TBA ambaye amechelewesha mradi huo kwa miaka yote ilihali wizara ya yenye dhamana ipo.

Alisema ujenzi wa jengo la maktaba katika chuo hicho, ulianza mwaka 2012 lakini haujakamilika kwa muda wa miaka saba.

Rais Magufuli alisema enzi za Hayati Mwalimu Julias Nyerere, chuo hicho kilijengwa kwa miaka minne kuanzia mwaka 1982 hadi mwaka 1986 lakini maktaba hiyo imejengwa kwa miaka saba na bado haijakamilika.

Aidha, aliahidi kusaidia kulipa deni linalodaiwa chuo hicho la Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya kumalizia kazi awamu ya pili na tatu ya ujenzi wa maktaba hiyo.

Alisema mkandarasi ameshalipwa Sh. bilioni 2.5 na bado hajapatiwa Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya kukamilisha kazi hiyo.

"Hizo Sh. bilioni 2.9 mwezi huu wa tano zitakuja zote sasa ole wenu mzichakachue. Tumuone na huyo mkandarasi kama atashindwa kumaliza kazi," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli aliahidi kutoa Sh. bilioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni ya chuo hicho ili kuwafanya wanafunzi wasome kwa uhuru.

Mbali na hilo, Rais Magufuli, aliwaagiza watendaji kumfukuza kazi mkandarasi raia wa China anayejenga barabara ya kuingia katika chuo hicho endapo ataendelea kusuasua kukamilisha mradi huo.

"Hela yote ipo, Sh. bilioni 10.4 ipo, tena mumwambie afanye kazi kwa saa 24 na huu mradi nitaufuatilia mimi. Wamezoea hawa watu wanaomba kazi wakipewa wanaanza kusua sua," Rais Magufuli alisema.

Aidha, alimwagiza Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, kupeleka ithibati ya mitaala ya kufundishia fani walizoomba chuo hicho ndani ya siku 10.

# Tucta yamwangukia Rais JPM nyongeza mishahara

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHIRIKISHO la Wafanyakazi Tanzania (Tucta) mkoani Manyara, limemwomba Rais John Magufuli kuongeza mishahara au kupunguza kodi kwa wafanyakazi ili kuwasaidia kuendana na gharama za maisha.

Mwenyekiti wa Tucta mkoani hapa, Talu Mohamed, alitoa ombi hilo Mei Mosi alipohutubia katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kwenye Uwanja wa Kwaraa.

"Kama kuna mkubwa nchi hii ni mfanyakazi, hebu nakuomba Mkuu wa Mkoa, baada ya sherehe hii zungumza na Mheshimiwa Rais, atuhurumie, atuongezee mishahara, hali zetu ni mbaya sana," Mohamed alisema.

Aliongeza kuwa kama serikali haiwezi kuongeza mishahara kwa sasa, basi wanaomba iwapunguzie kodi, akidai kuwa inayotozwa ni kubwa na hawana mbinu ya kuikwepa.

"Tunaomba atuhurumie sisi na tunamsihi sana atuhurumie katika hili, naomba mkuu wa mkoa mpe taarifa hizi Mheshimiwa Rais," alisema.

Kiongozi huyo wa Tucta pia aliiomba serikali kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi ili kuepuka kuwavunja moyo wa kufanya kazi.

Awali, Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (Tughe) Mkoa wa Manyara, Saburi Yakubu, alimpongeza Rais kwa kuwarejeshea wafanyakazi mafao yao kwa kuagiza kitumike kikokotoo cha zamani katika tamko lake la Desemba 28, mwaka jana.

Hata hivyo, alisema bado wanakabiliwa na changamoto za baadhi ya waajiri kutokufuata taratibu za kinidhamu, kutokuwapandisha vyeo na madaraja toka mwaka 2015 na baadhi ya halmashauri mabaraza ya wafanya kazi yameisha muda wake na wanadai malimbikizo ya posho zao.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, akijibu baadhi ya hoja za wafanyakazi hao, alisema anafikiri uwapo mkakati wa kupunguza mfumko wa bei ambao unasababisha wafanyakazi walie hali ngumu ya maisha.

Alisema serikali iko kwenye kipindi cha mabadiliko, hivyo kulipana mishahara mikubwa hakutasaidia kuiendesha nchi kwa kuwa Tanzania ni kubwa na wafanyakazi ni wengi.

Mnyeti alisema hajaona mfanyakazi wa umma ambaye amekata tamaa kwa kutokuongezewa mshahara, badala yake wote wanaendelea kuchapa kazi kwa lengo la kuliletea taifa maendeleo.

"Waajiri wote hapa, yaani wakurugenzi wanatakiwa kuheshimu sheria za kazi na kama kwa yale mabaraza ya wafanyakazi ambayo yameisha muda wake, yaanzishwe haraka sana ili yaweze kusaidia kutetea haki za wafanyakazi," Mnyeti alisema.

Alitumia fursa hiyo kuvionya vyama vya wafanyakazi, kutokuwa sehemu ya kuchochea migomo na kutogeuzwa vyama vya siasa.



Mwanafunzi wa Shule ya msingi Naurei, Kata ya Kiutu, katika Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, akipokea dawa kutoka kwa mganga wa halmashauri hiyo, wakati wa zoezi la siku mbili la kutoa kinga na tiba ya kichocho na minyoo kwa watoto chini ya miaka mitano, lililofanyika shuleni hapo juzi. **PICHA: ALLAN ISACK**

# Waziri Mkuchika aagiza waajiri kuthamini makatibu mahsusi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, amewaagiza waajiri wa umma na binafsi nchini, kuruhusu makatibu mahsusi kujiendeleza kitaaluma na kuhudhuria mkutano wa chama chao (Tapsea) kinachofanyika mara moja kwa mwaka.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha alipofungua mkutano wa saba wa Tapsea kilichohudhuriwa na washiriki 2,300 kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema hakuna sababu ya kuwazuia kuhudhuria mkutano huo ilhali unafanyika mara moja kwa mwaka na huko wanapata elimu ya kuboresha utendaji kazi wao kwa faida ya nchi.

"Sisi viongozi tunaozuia hawa makatibu mahsusi wetu ambao wanasafiri mara moja kwa mwaka, tujiulize sisi tunasafiri mara ngapi kwa mwaka, naomba tuache hii tabia, tuwaruhusu wakajiendeleze na kushiriki mikutano yao," Mkuchika aliagiza.

Alisema chama hicho kimesajiriwa na serikali, hivyo kila mmoja lazima akiheshimu na kuhusu makatibu mahsusi wake kushiriki mikutano kinayoiandaa.

Aliwataka makatibu mahsusi kujiendeleza kitaaluma ili waboreshe kazi zao na kuendana na mahitaji ya wakati.

Alikipongeza chama hicho kwa kuchangia damu salama ili kusaidia jamii ya Tanzania.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Seif Shaaban Mwinyi, alisema makatibu mahsusi ni muhimu katika utendaji kazi wa serikali.

Alisema serikali iko tayari kutoa ushirikiano kukisaidia chama chao kufanikisha malengo yake.

"Kwa upande wa Zanzibar, mwamko kwa makatibu mahsusi sasa ni mkubwa ndiyo maana mwaka jana, walipofanya mkutano huo Zanzibar, walishiriki 18 tu na mwaka huu wameongezeka hadi zaidi ya 90 walioshiriki mkutano huu wa saba," alisema.

Mwenyekiti wa Tapsea, Zuhura Maganga, alitumia fursa ya mkutano huo kuiomba serikali kuongeza mishahara yao ambayo kwa sasa wanalipwa midogo isiyolingana na kazi wanazofanya.

Vilevile, aliiomba serikali itoe nafasi kwa Tapsea kuwa wajumbe wa bodi katika Chuo cha Utumishi wa Umma kilichoko Magogoni jijini Dar es Salaam ili iwe rahisi kufikisha maoni ya kada hiyo kirahisi. "Lakini, tunaomba pia waajiri waruhusu kusoma na kuwalipia makatibu mahsusi katika ngazi ya shahada ya uzamili," alisema.

# DC atoa mwaka ujenzi makao makuu halmashauri

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

MKUU wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga, ameitaka Kampuni ya Mzinga Holding inayoendesha ujenzi wa jengo la makao makuu ya halmashauri ya wilaya hiyo, kujenga kwa ubora na kukamilisha mradi kabla ya Aprili Mosi mwakani.

Mofuga alitoa agizo hilo jana alipozindua mradi huo unaotekelezwa katika Kata ya Dongobesh.

Alisema anatarajia ujenzi huo utakwenda kwa kasi na kumalizika kabla ya Aprili Mosi mwakani ili watumishi wa halmashauri hiyo wawe wamehamia na kufanya kazi ya kuhudumia wananchi kwa karibu zaidi.

"Mzinga malizeni jengo kwa wakati kwani fedha za ujenzi zipo na sisi tunawashukuru viongozi wa dini kwa kumwombea Rais (John) Magufuli kwani maendeleo aliyoyafanya Tanzania, utadhani amekaa madarakani kwa zaidi ya miaka 40," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Hudson Kamoga, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa jengo hilo.

Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay (CCM), alisema utekelezaji wa mradi huo utasogeza huduma ya jamii karibu zaidi na wananchi wa jimbo hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Joseph Mandoo, alisema madiwani wa halmashauri hiyo ndiyo waliamua makao makuu yawe Dongobesh, baada ya wataalamu kupendekeza eneo hilo.

Mandoo alisema wataalamu hao waliagizwa na madiwani wafanye utafiti wa kata inayofaa kuwa makao makuu ya halmashauri hiyo.

Mkazi wa Kata ya Dongobesh, Elizabeth Bayo, alisema ujenzi wa makao makuu ya halmashauri ya wilaya hiyo utachochea zaidi uchumi wa wananchi wa eneo hilo.

Mhandisi Mkadiriaji wa Majengo wa Kampuni ya Mzinga Holding, Alex Shedrack, alisema jengo hilo litajengwa kwa Sh. bilioni 4.7 na wanaamini watakamilisha mradi kufikia Aprili Mosi mwakani.

# Wengine wawili waikimbia Chadema

**Mary Mosha na Paul William,**

MOSHI

HALI bado sio nzuri ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) katika Jimbo la Moshi vijijini baada ya madiwani wawili mmoja akiwa wa Viti Maalum kujiuzulu nafasi zao na kujiunga na Chama cha Mapinduzi (CCM).

Diwani wa Kata ya Uru Shimbwe, Bertin Mkami na wa Viti maalum kupitia kata ya Uru Mashariki, Elizabeth Temba, walieleza kuwa sababu zilizowafanya kujiuzulu na kutimkia CCM ni kutokana na kuchoshwa na migogoro ndani ya Chadema.

Akiwapokea madiwani hao jana katika Ofisi za CCM mkoa, Mwenyekiti wa CCM mkoa, Patrick Boisafi, alisema kuwa, ni furaha kwa chama hicho kuona wanachama waliotoka katika uchaguzi wa mwaka 2015 wanarejea.

Boisafi alisema kuwa, wanachama hao wameona kazi zinazofanywa na serikali ya awamu ya tano kupitia ilani ya uchaguzi yenye malengo ya kuwakomboa Watanzania na wao wameamua kuunga mkono kazi hizo.

Alisema kuwa, ndani ya Chadema kwa sasa ni malumbano yasiyoisha, sio malengo ya chama chochote cha siasa na kuwataka viongozi wengine wa Chadema watakaoshindwa kuvumilia hali hiyo kurudi katika chama chenye nia ya kuwaatumikia wananchi na kuahidi kuendelea kuwapokea.

Diwani wa kata ya Uru, Shimbwe Mkami, alisema kuwa Chadema kumekuwa na migogoro ndani ya chama hicho isiyoisha na amemtuhumu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Michael Kilawila ndio amekuwa chanzo cha migogoro hiyo.

"Migogoro ndani ya Chadema inayolelewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Kilawila imekuwa chanzo cha kusababisha maendeleo ya kata yangu kurudi nyuma na mimi nilichaguliwa na wananchi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo na sio migogoro," alisema Mkami.

Diwani huyo aliongeza kuwa, tokea kuchaguliwa kwa Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini, Antony Komu pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Moshi, Michael Kilawila mwaka 2015 hawajawahi kufika katika kata yake kwa ajili ya kusikiliza matatizo yanayowakabili wananchi ili waweze kuyatatua.

Naye Diwani wa Viti Maalum, Elizabeth alisema kuwa, ameamua kutoka Chadema na kuhamia katika chama chenye malengo ya kuwatumikia wananchi kikiongozwa na Ilani yake ambacho ni CCM. Alisema kuwa, Chadema ni chama ambacho kimekuwa kikijali maslahi ya baadhi ya viongozi badala ya wananchi ambao ndio waliowachagua ili waweze kuwatumikia.

Alipotafutwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi, Kastori Msigala, kuzungumzia kama alishapokea barua za madiwani hao wawili kujiuzulu, alikiri kupokea na kusema kuwa wameshatuma barua Wizara ya Tamisemi kujulisha kata ya Uru Shimbwe kuwa wazi pamoja na nafasi moja ya diwani wa viti maalum.

"Kutokana na madiwani hawa wawili kujiuzulu kunaifanya halmashauri yetu kuwa na kata mbili zilizo wazi ambazo ni Uru Shimbwe pamoja na kata ya Kibosho Magharibi na nafasi moja ya diwani wa viti maalum," alisema Msigala.

Kuondoka kwa madiwani hao kunafanya idadi ya waliojiuzulu nyazifa zao kutoka Chadema na kujiunga na CCM kufikia 20 katika Mkoa wa Kilimanjaro tangu kufanyike kwa uchaguzi mkuu mwaka 2015




Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari wa Mkoa wa Manyara (MAMEC), Yusuph Dai (kushoto), akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani mjini Babati juzi, Kulia ni Katibu wa MAMEC, Theddy Charle na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamis Malinga. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi Karanga wataka ulinzi shirikishi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKAZI wa Kata ya Karanga, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wamemuomba Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Anna Mghwira, kuingilia kati suala la ulinzi na usalama wa kata hiyo kutokana na kukithiri kwa matukio ya kihalifu huku viongozi wa kata wakishindwa kuwajibika.

Wakizungumza na Nipashe, Mary Costantine, alisema kumekuwapo na matukio ya kihalifu yanayoongezeka katika kata hiyo huku wakiwatuhumu viongozi wa kata hiyo kujibu majibu ya jeuri na dharau mara wanapoenda kuomba msaada wa changamoto hizo.

Alisema matukio hayo ya kihalifu yamekithiri kutokana na ongezeko la vichaka virefu pembezoni mwa barabara licha kuwa kata hiyo ni miongoni mwa zilizopo katika Manispaa ya Moshi.

Ernest Msofe, alisema mbali na kuwapo kwa vichaka pembezoni, pia wapo watu ambao sio waaminifu wamekuwa wakiuza na kutumia madawa ya kulevya kwa vijana.

"Tumechoka na matukio haya, katika kipindi cha mwezi moja uliopita, wapo baadhi ya kinamama wameporwa fedha na hata wengine kubakwa katika eneo la Kilimani huku viongozi wa kata wakiwa wameufumbia macho uhalifu huo," alisema Msofe.

Shabani Mkure, alidai matukio mengine yanatokea na wanapoenda kutoa taarifa katika uongozi wa kata wanayapuuzia kutokana na watendaji hao asilimia kubwa hawakai katika kata hiyo.

"Sisi tunamuomba Mkurugenzi wa Manispaa kutupa Mtendaji ambaye kwanza mwenye utayari wa kusikiliza kero za wananchi kwa wakati na ikiwezekana anayeishi katika kata hiyo ili kujua uchungu wa matukio yanayotokea na kuchukua hatua kwa wakati," alisema.

Hata hivyo, Nipashe ilimtafuta mtendaji wa kata hiyo, Leocardia Moswary ili kujibu changamoto zinazowakabili wananchi, lakini alisema hayupo tayari kuzungumza kwa sasa.

"Kwa sasa nipo darasani siwezi kuongea chochote na ikiwa una ashida yoyote nenda kwa watendaji wa mitaa au balozi wako," alisema.

Hata hivyo Nipashe ilimtafuta Diwani wa kata ya Karanga, Jonathan Makupa na alipoelezwa kuhusu changamoto hizo, alisema kwa sasa kwenye kata hiyo hakuna polisi jamii, lakini amelichukuwa na atalifanyia kazi kwa wakati.

"Nimepokea changamoto za wananchi, ni kweli kwenye kata yetu kwa sasa hatuna polisi jamii ila nimeyachukua na nitayafanyia kazi na hali ya usalama itarejea kama ilivyokuwa mwanzo... nawaomba wananchi wawe wavumilivu na watoe ushirikiano ili tuweze kuwabaini hao wahalifu," alisema.

## Waandishi walilia bima kuwalinda kazini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KLABU ya waandishi wa habari mkoani Kilimanjaro (Mecki), imeomba serikali kuingilia kati ili kuwapo kwa maslahi mapana ya wanahabari katika vyombo wanavyofanyia kazi hususani suala la bima za maisha.

Aidha, vyombo vya habari vimeombwa kusaidia hata kwa mkopo kuwasomesha waandishi wa habari wenye sifa za kujiunga vyuo vikuu nchini.

Katibu wa Mecki, Nakajumo James, alisema hayo wakati akizungumzia Siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani inayoadhimishwa kila mkoa hapa nchini huku kitaifa ikifanyika jijini Dodoma.

"Waandishi wa habari ni watu muhimu sana na pengine muhimili wa nne usiotajwa kikatiba, ila wanafanya kazi katika mazingira magumu na hata kutishiwa maisha na wengine kupotea, tunahitaji serikali iliangalie hili ili tuendelee kuisaidia katika kufichua na kuibua yanayofichwa," alisema.

James alitaka kuwapo kwa mikataba ya ajira, maslahi bora, uhuru wa kutoa maoni hata yale yanayoonekana kukosoa mamlaka, lakini pia kuwasaidia kuongeza viwango vya elimu.

"Kwa Mkoa wa Kilimanjaro tumeona tuadhimishe kwa kuzungumza na vyombo vya habari, lakini wiki ijayo tutakaa na wakurugenzi wa halmashauri za wilaya ili watuhakikishie wanahabari kushiriki wakati wa kampeni na uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu mwakani."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mecki, Bahati Mustapher, alisema maadhimisho ya mwaka huu pia ni sehemu ya wanahabari kujitathmini mwenendo wao na kama wanatekeleza matakwa ya kitaaluma na sheria za nchi.

Alisema maadhimisho ya mwaka huu, yamebeba ujumbe, Usalama wa mwandishi wa habari katika kipindi cha uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu 2020.

Nao baadhi ya waandishi, Upendo Mosha na Omary Mlekwa, waliomba wanahabari kuzingatia maadili ya taaluma yao ili kuepuka kusigana na serikali bila sababu za msingi.






Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abassi (kulia), akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma jana. Wengine ni Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini, Inmi Patterson (kushoto) na Balozi wa Uingereza hapa nchini, Sarah Cooke. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kundecha awaasa wanawake kudhalilishwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWENYEKITI wa Baraza la Maulamaa nchini, Sheikh Mussa Kundecha, amewataka wanawake wa kiislamu kupinga vitendo vyote ambavyo vimekuwa vikidhalilisha utu wao kwa manufaa ya watu wengine.

Kundecha aliyasema hayo wakati akizungumza na waumini wa dini hiyo katika kongamano la kuukaribisha Mwezi wa Ramadhani lililoandaliwa na Taasisi ya kiislamu, ya Kalamu Education Foundation (KEF).

Sheikh Kundecha, alisema wanawake wa kiislamu wanatakiwa kupinga vitendo vyote ambavyo vimekuwa vikifanywa katika maeneo mbalimbali ambavyo vimekuwa vikiudhalilisha utu wao.

Alisema wanawake wamekuwa wakitumika katika mambo mbalimbali ya ovyo ambayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya watu kwa maslahi yao binafsi.

"Leo hii kila jambo la ovyo anayetumika ni mtoto wa kike, ukikuta tangazo la biashara anakuta kawekwa mwanamke, lakini akiwa hana hata nguo za kumsitili, hivyo basi kinamama wa kiislam lazima tubadilike na kupinga hivi vitu vinavyoudhalilisha utu wetu," alisema.

Naye Dk. Mbaraka Ahmed Awes, kutoka Nairobi Kenya ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema moja ya changamoto kwa kinamama wa kiislam ni ujio wa mila za mataifa ya magharibi katika nchi zinazoendelea kama Tanzania.

Alisema kutokana na ujio wa mila za mataifa hayo pamoja na mabadiliko ya sayansi na teknolijia kumechangia hata ndoa nyingi za waislamu kuvunjika.

"Unakuta leo hizi tamthilia tunazo angalia majumbani kwetu zinachangia kwa kiasi kikubwa kuvunja ndoa zetu majumbani mwetu eti tu mwanamke wa kiislamu na yeye anataka kuishi kama ambavyo waingizaji wa tamthilia wanavyoishi bila kujua kuwa ule sio uhalisia wa maisha yao" alisema.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Awes alitoa rai kwa wanawake wa kiislam kubadilika na kuishi kama ambavyo walikuwa wakiishi zamani.

"Kinamama ndiyo walezi wakuu wa familia zetu hivyo basi kama leo hii wataendelea hivi basi tutakuwa na kizazi cha ajabu sana ambacho hakina maadili mema ya kiafrika," alisema.

Naye Mhadhiri wa chuo cha Kiislamu cha Morogoro, Dk. Mohammed Dedes, akitoa mada katika kongamano hilo aliwataka waislamu kujijengea tabia ya kwenda hija.

Alisema kwenda hija ni jambo la muhimu kwa mwislamu, hivyo ni lazima wakawa wanajiwekea akiba ili kutimiza moja kati ya nguzo ya dini yao na matakwa ya mtume wao.

# Wafamasia wataka kibano uuzaji dawa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAFAMASIA mkoani Dodoma wameiomba serikali na Baraza la Wafamasia nchini kuongeza usimamizi wa sheria zinazowabana wauzaji wa maduka ya dawa nchini.

Hatua hii imekuja kufuatia kuwapo kwa maduka mengi yanayouza dawa za binadamu kutoa dawa za anti-biotic kiholela bila kufuata taratibu za kifamasia na kusababisha watumiaji wengi kuwa na usugu wa dawa.

Hayo yamebainishwa jana jijini hapa na Mkuu wa Idara ya Wafamasia wa Hospitali ya Rufani mkoa wa Dodoma, Nelly Shiletiwa, katika ufunguzi wa semina ya iliyolenga kuwajenga watoa huduma za afya kuwa sehemu ya utatuzi wa usugu wa vimelea vya magonjwa katika jamii.

Alisema usugu wa vimelea vya magonjwa ni hali ya dawa kushindwa kudhibiti magonjwa na kuviua, hali inayosabaisha dawa kushindwa kufanya kazi na kutoa matokea yanayotarajiwa.

"Tuiombe serikali na wadau wa afya kusimamia kwa ukaribu zaidi juu utoaji wa dawa katika maduka ya mitaani ili kuzuia tatizo la usugu wa dawa," alisema na kuongeza: "Ifahamike kuwa vimelea vya magonjwa ndivyo vinakuwa sugu dhidi ya dawa na kusababisha kukwamisha juhudi za utoaji huduma bora za afya."

Mkufunzi katika mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha St. John, Romuald Mbwasi, alisema tatizo la usugu wa dawa linaleta madhara kwa binadamu, mifugo na hata mimea, na kusababisha kushindwa kutibu ipasavyo.

Alitaja moja ya sababu zinazosababisha usugu wa vimelea vya magonjwa kuwa ni pamoja na matumizi yasiyo sahihi.

Alitaja sababu nyingine ni kutozingatia kanuni za usafi kama unawaji wa mikono na kununua dawa zenye kupaswa kutolewa na cheti cha daktari. "Baadhi ya madhara yatokanayo na usugu wa vimelea vya magonjwa ni vifo kwa binadamu, mifugo na mimea ambapo takribani watu 700,000 hufariki duniani kutokana na tatizo hili kila mwaka," alisema Mbwasi.

Mwandaaji wa mafunzo hayo ambaye ni mtendaji mkuu wa shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na utoaji wa elimu juu utatuzi wa usugu wa vimelea vya magonjwa katika jamii (RBA INITIATIVE), Erick Venant, alitahadharisha kuwa kama juhudi za haraka zizisipochukuliwa na wadau wa afya, vifo vitokanavyo na tatizo hilo vitaongezeka hadi kufikia watu milioni 10 kwa mwaka ifikapo mwaka 2050.

## Alia ongezeko tozo ya mafuta

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Muheza (CCM), Adadi Rajabu, amesema ongezeko la tozo ya Sh.100 kwenye mafuta kwa ajili ya mfuko wa maji limekuwa likipigiwa kelele sana kwa miaka mitatu ni vyema likatekelezwa. Akichangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2019/20, Mbunge huyo alisema awali tozo hiyo ilikuwa Sh.50 kwasasa inapendezwa tozo hiyo inatakiwa kuongezwa ili kufikia 100. "Hii ni kutokana na fedha ambazo zinapatikana zinazolipa wakandarasi kwa sasa zinaonekana zimetoka kwenye mfuko wa maji wa taifa hivyo umesaidia na kuondoa upungufu wa wizara kuonekana haina hela..Lakini umesaidia kulipa malipo mbalimbali lakini hazitoshi,"alisisitiza.

Aidha, alisema kuwa Muheza wana mradi ambao unatoa maji kutoka Tanga Pongwe hadi mjini Muheza ili kuondoa tatizo la maji kwenye jimbo hilo.

Alisema mradi huo ulitegemewa kumalizika tangu mwezi Mei mwaka jana lakini hadi sasa bado unaendelea kujengwa na upo kwenye asilimia 70.

"Kazi kubwa inafanyika lakini mradi huu ambao tunautegemea ulikuwa kwenye mpango wa huo ili kupunguza tatizo la maji Muheza sasa hivi kama nilivyosema imebaki kitu kidogo sana kwamba asilimia 30 ili maji yatiririke Muheza ingawaje haitakidhi sehemu kubwa,"alisema

Adadi alisema tatizo lililobaki ni kufumua mabomba yaliyochakaa mjini Muheza na kuweka mapya na kwamba suala hilo limesitishwa kidogo kusubiri mradi mkubwa wa maji kutoka Nchini India wa dola za marekeni milioni 500.

Alisema amezungumza na Waziri husika kuhusu suala hilo na kwamba anamuomba na kusisitiza kuwa waruhusu sasa hivi ili mabomba hayo yaanze kufumuliwa kwa sababu tenki ambalo lilikuwa linachelewesha limekwisha tengenezwa na limekaribia kukamilika. Alisema kwenye bajeti ameona imepangwa zaidi ya milioni 700 hivyo alimwomba Waziri aruhusu wakati mradi mkubwa unasubiriwa mabomba hayo yaanze kufumuliwa ili mkandarasi aanze kazi na maji yapatikane wakati wanasubiri mradi hu mkubwa.

"Baada ya kutangaza basi mruhusu moja kwa moja ili wapatikane wakandarasi watie saini badala ya kusubiri irudi Wizarani kuomba kibali kingine," alisema





# Shein asisitiza mahali pazuri pa kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kuwa na mahali pazuri pa kufanyia kazi kunampelekea mtendaji afanye kazi kwa furaha, umakini na kujiamini zaidi.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa jengo la Ofisi za Serikali huko Gombani Chake Chake Pemba, Mkoa wa Kusini Pemba, alisema Serikali imejenga ofisi hizo ili kurahisisha utoaji wa huduma hivyo, kila mfanyakazi ahakikishe anawajibika ipasavyo kulingana na dhamana na majukumu ya kazi aliyopangiwa.

Dk. Shein aliwataka wafanyakazi wahakikishe wanatumia vizuri muda wa kazi kwa kufanya mambo yanayopaswa kufanywa katika sehemu za kazi.

Alieleza kuwa miongoni mwa malengo makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuona watumishi wa umma wanafanya kazi zao katika mazingira bora na salama zaidi.

Rais Dk. Shein alisema kuwa uzinduzi wa jengo hilo ni miongoni mwa vielelezo muhimu vya utekelezaji wa lengo hilo.

Alisema ujenzi wa jengo hilo ni jitihada za Serikali kupitia maamuzi ya Baraza la Mapinduzi na lengo ni kuwawezesha wafanyakazi katika mazingira mazuri.

Alieleza kuwa ujenzi huo unatokana na baadhi ya ofisi kuchakaa, nyingine hazina nafasi ya kutosha kwa ajili ya watumishi pamoja na wananchi wanaofika kwa ajili ya kupatiwa huduma.

Alisema kuwa Serikali itaongeza mshahara kwa kima cha chini na juu pale mapato yatakapoongezeka kwa wafanyakazi kuzidi kujituma na kuendelea kufanya kazi kwa ari, taratibu na nidhamu.

Aliwataka wafanyakazi kufanya kazi kwa saa nane za kazi kwa siku kwani hatua hiyo itaongeza ufanisi na kuongeza mapato, huku akisisitiza haja kwa wafanyakazi kutunza siri za kazi kwa kuwa ni nyenzo kubwa katika utawala bora sambamba na kujiepusha na malumbano.

Aliongeza kuwa kuna haja ya kutafuta namna itakayowezesha kudhibiti matumizi ya simu za mikononi wakati wa saa za kazi kwa kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi katika sehemu mbalimbali juu ya suala matumizi mabaya ya simu.

"Wafanyakazi wanatumia muda mwingi kazini kuchati na kuperuzi katika mitandao ya kijamii.. vile vile natoa tahadhari kwa wale wanaotega kazi kwamba kuwapo kwa ofisi hizi ndani ya jengo moja kusichukuliwe kuwa ni ukaribu wa marafiki kuonana kirahisi kwa ajili ya mazungumzo," alionya.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, alisema ujenzi wa jengo hilo lenye vyumba 145, umegharimu jumla ya Sh. bilioni 13.6 ambazo ni fedha za mapato ya Serikali.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Mwakilishi wa UNICEF nchini Tanzania, Maniza Zamani, alipokwenda Ikulu Zanzibar jana, kuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi nchini. Kushoto ni Mwakilishi wa UNICEF anayefanya kazi zake Zanzibar, Maha Damaj. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mkakati mpya kumaliza Ukimwi 2030

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kumaliza janga la Ukimwi Zanzibar, Shirika la Amref limezindua mradi mpya unaolenga kupanua juhudi za utoaji wa huduma za matunzo na matibabu ya kufubaza kirusi (VVU) ili kumaliza janga hilo ifikapo 2030.

Uzinduzi wa mradi huo ujulikanao Afya kamilifu ulifanyika Maruhubi Mjini Zanzibar na kuzinduliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Asha Abdallah Ali.

Akizungumza baada ya kuzindua mradi huo, alisema Serikali itaendelea kuunga mkono jitihada za shirika hilo lenye lengo la kupambana na Ukimwi Zanzibar.

Aliliomba shirika hilo kuongeza nguvu zaidi katika makundi maalum kwa kuwa bado maambukizi ni makubwa kulinganisha na watu wa kawasaidia.

Aliyataja makundi hayo ni watumiaji wa dawa za kulevya wanaojidunga sindano, wanawake wanaofanya biashara ya ngono na wanaume wanaofanya mapenzi ya jinsia moja.

Aidha, alisema Zanzibar ina asilimia moja ya kiwango cha maambukizi na hiyo inatokana na juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kupambana na ungojwa huo.

Alilitaka shirika hilo katika kutekeleza mradi huo kuziwezesha serikali za mitaa ili nazo zishiriki katika kutoa elimu katika ngazi za shehia ili wananchi waweze kujilinda.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Amref Health Africa, Florence Temu, alisema mradi huo wa afya kamilifu unalenga kuongeza idadi ya watu wanaojijua kuwa wanaishi na VVU na Ukimwi wanapata huduma za upimaji wa VVU na ushauri, matunzo na matibabu ya kufubaza virusi ili kuhakikisha kwamba vinafubazwa.

"Hadi kufikia mwisho wa mradi tunalenga kuhakikisha kwamba watu wote wanaoishi na VVU na Ukimwi watakua wanajua hali zao na wanapata matibabu," alisema.

Kwa upande wake, Meneja wa mradi huo, Edwin Kilimba, alisema kwa zaidi ya miaka 30 shirika la Amref Afrika limekuwa likishirikiana na serikali ya Tanzania na wadau wengine kuimarisha mifumo ya afya nchini ili kuondoa changamoto zinazochochea kurudisha nyuma maendeleo.

## Wanahabari wapewa onyo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Juma Nhunga, amewataka waandishi wa habari kutotumia kalamu zao kuwaumiza watu wengine ambao hawana uwezo wa kutumia majukwaa ya kihabari kujitetea.

Aliyasema hayo katika maadhimisho ya siku ya uhuru wa vyombo vya habari yaliofanyika ukumbi wa sanaa Rahaleo Mjini Unguja.

Alisema waandishi wa habari pamoja na kuripoti masuala ya kawaida yanayoihusu jamii, wazingatie kuandika habari zitakazoibua hoja katika masuala ya uhujumu wa uchumi, utakatishaji fedha na udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema iwapo mambo hayo yataibuliwa, yatasaidia kuchuchea kasi ya maendeleo na ustawi wa jamii.

Aidha, alizipongeza taasisi za kihabari na vyombo vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya na kuwataka kuendelea kufanya kazi zao kwa kuzingatia weledi na maadili ya uandishi wa habari.

"Serikali ya Zanzibar inaheshimu na kuthamini kazi kubwa mnayoifanya na napenda kuwahakikishia kwamba itaendelea kutoa uhuru kwa vyombo vya habari," alisema.

Akitoa tamko la wadau katika maadhimisho hayo kwa niaba ya kamati ya maandalizi ya maadhimisho hayo, Dk. Juma Muhammed Salum, alisema pamoja na kuwapo kwa uhuru wa habari, bado kuna changamoto mbalimbali zinazoashiria ukiukwaji wa uhuru wa vyombo vya habari Zanzibar.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo ni kutokuwapo kwa sheria mahususi ya habari na vyombo vya habari, kukosekana kwa vyama vya wafanyazi wa waandishi wa habari na malipo duni yasiyozingatia sheria za serikali kwa baadhi ya vyombo vya habari kwa waandishi wake.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) ofisi za Zanzibar, Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar, Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar na Udara ya Habari (Maelezo) Zanzibar.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**WEMA HATAKI TENA WAPIGA MIZINGA** Soma UK.19

JUMAMOSI MEI 4, 2019



# 'Nimenasa' yawaunganisha Amin, Linah

## BASI SAWA



# We Voice Wonder punguza miyeyusho

BAADA ya kuahirisha mara kwa mara ujio wake mpya, msanii Voice Wonder, amesema sasa ataanza kazi rasmi mwezi huu wa Mei.

"Nilipanga kuanza januari nikaahirisha hadi Aprili, lakini mambo yakaenda ndivyo sivyo, sasa nitaanza kazi rasmi mwezi huu," amesema Wonder.

Msanii huyo amesema ataanza kwa wimbo wa 'Kitu Kimba' ambao anamini utatambulisha vizuri ujio wake mpya baada ya kimya cha miaka mingi.

Amewaomba radhi mashabiki wake kutokana na jinsi ambavyo amekuwa akiahidi na kuahirisha ujio huo na kusema sasa hatarudi nyuma tena.



# Ziba masikio fuata soko Mashauzi

NYOTA wa muziki wa taarab Isha Mashauzi amefunguka kuwa analazimika kuvaa suruali kwenye muziki huo ili kuendana na soko linavyotaka.

"Kuna watu wanachonga sana kuniona nimevaa suruali kwenye nyimbo zangu za muziki wa taarab, wajue kuwa mimi ni msanii, ni lazima ubadilike kuendana na soko la muziki," amesema Mashauzi.

Mbali na hilo, amesema yeye siyo mpenzi wa kutunga nyimbo za kuwashambulia watu wengine bali ni za kumsifia zaidi mama yake mzazi, Rukia Juma, kwa vile anampenda sana.



# 'Nimenasa' yawaunganisha Amin, Linah

WASANII, Amin Mwinyimkuu na Linah Sanga wamefyatua video ya kibao chao kipya kiitwacho 'Nimenasa' ikiwa ni maandalizi ya albamu yao mpya.

Amin ameiambia BT kuwa video hiyo imechukuliwa mwanzoni mwa wiki hii katika Wilaya ya Lushoto na vitongoji vyake mkoani Tanga.

"Tumeamua kwenda Lushoto ili kutangaza utalii wa ndani, siyo kukimbilia nje ya nchi kama wanavyofanya baadhi ya wasanii," amesema Amin.

Msanii amesema baadhi ya watu wamekuwa wakidhani kwamba huenda wawili hao ambao wamewahi kuwa wapenzi wamerudiana na kufafanua kuwa hilo halina ukweli wowote.

"Hapa ni kazi tu, kila mtu ana 'time' yake kwani mambo ya mapenzi yalikwisha tangu mwaka 42 sisi hapa tunaandaa albamu ya pamoja tu," amesema.

Amesema wanaofuatilia muziki wa kizazi kipya wanajua uwezo wa Linah katika muziki na kwamba ndio maana ameamua kumshirikisha ingawa kuna wasanii wengi wa kike nchini.

## INSTA-TWITTER





**Kila mwanamume** anatakiwa angalau awe na suti moja hivi matata **- Dogo janja.**



**Ukiota** ndoto hazina rangi amka uzipake mwenyewe.. Nawaombea wiki njema watu wa Mungu **- Mwana FA.**



# Wema hataki tena wapiga mizinga

MWIGIZAJI wa filamu, Wema Sepetu, ametafakari kwa kina na kuamua kufyekelea mbali watu wasio na faida kwake ili kulinda 'brandi' yake.

Amesema kwa muda mrefu alikuwa na 'kampani' ya watu wanaomnyonya, bila yeye kupata faida kwao na kujikuta akiharibiwa mipango ya uigizaji.

"Ninapenda uigizaji kuliko kazi nyingine, lakini bahati mbaya 'kampani' za watu wasio na msaada wowote zimenipotezea muda, sitaki kuwa nazo tena," amesema Wema.

Amesema ametumia miaka zaidi ya mitatu 'kujibrandi', lakini 'kampuni' zilitaka kumfanya aonekane mtu wa ajabu mbele ya jamii kwa kumuingiza katika mambo yasiyofaa na pia kumpiga 'mizinga'.




>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow

@burudanitele

## UNASEMAAA...

# Beka Flavour: Sitaki kushindanishwa

BEKA Flavour, ambaye kwa sasa ni miongoni mwa wasanii ambao wako matawi ya juu, amesema hataki kushindanishwa katika muziki wa kizazi kipya.

"Baadhi ya wadau wa muziki wa kizazi kipya wamekuwa wakitamani kunishindanisha na wasanii wengine...sitaki kushindanishwa na watu wengine, muziki wangu unatosha kunitangaza," amesema Beka.

Amesema hajawahi kufikiria kufanya kazi kwa kutegemea kushindanishwa ili kupata umaarufu na kudai kwamba umaarufu alionao unamtosha.



# Huo ni uamuzi sahihi Nuh Mziwanda

MSANII wa muziki wa Bongo, Nuh Mziwanda, amesema kila siku anamuomba Mwenyezi Mungu aweze kupata mke ambaye atadumu naye katika ndoa.

"Nimeamua kumwachia Mungu ili aweze kunipa mke mwema, nitakayeishi naye kwa shida na raha katika ndoa, kila siku ninaomba iwe hivyo," amesema Nuh.

Amesema njia nzuri ya kufanikiwa kupata mke mwema ni kumshirikisha Mungu kwa vile anajua yeye (Nuh) kama binadamu hawezi kufanikiwa bila kumuweka Mungu mbele.

"Nimekuwa nikiulizwa kwanini sina mke, jibu langu ni kwamba bado nina mpango wa kuoa, lakini kikubwa zaidi ninamuomba Mungu anipe mke mwema,|" amesema.



## BODA 2 BODA

# Saida Karoli sasa hadanganyiki

SAIDA Karoli amesema kwa sasa yuko makini kutafuta wasimamizi wa kazi zake ili asijikute akiangukia mikononi mwa watu wanaonufaika kwa jasho lake.

Msanii huyo wa nyimbo za asili ambaye anaishi jijini Mwanza, amesema alikuwa na mpango wa kuhamia Dar es Salaam, lakini amekwama kwa sababu ya kukosa msimamizi wa kazi zake.

"Mwanzoni mwa mwaka 2000 nilikuwa na umaarufu mkubwa katika muziki wa asili hadi nikawa ninapata maonyesho mengi ndani na nje ya nchi, lakini walifaidika wengine. Kwa sasa niko makini katika kutafuta wasimamizi wa kazi zangu ili nisiendelee kutapeliwa," amesema Saida.




## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
@burudanitele



**Kulingana** na mambo ninayoyaona mtandaoni, nashangaa sana wanaume wanaowashusha wanawake, mbona hii kazi hawajatuomba msaada, wanaifanya vizuri kabisa wenyewe kwa wenyewe. Wacha nipite zangu - **Idriss Sultan.**



**Kwenye** maisha tunakutana na mitihani mingi na kuishinda, na huwa naamini Mungu huwapa Mapambano magumu waja wake nakwa wale walio imara hupita salama - **Elizabeth Michael Lulu.**



**Heshima** unayopewa Leo ukiweza kuiheshimu na wewe unaweza kufika malengo - **Steve Nyerere.**

# Kuumbe!

## Lutumba Simaro kuzikwa kesho Kinshasa



**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI wa siku nyingi nchini Congo DR na barani Afrika, Lutumba Simaro Masiya, aliyefariki nchini Ufaransa Machi 30, sasa anatarajiwa kuzikwa kesho Mei 5 nchini kwao.

Mwili wa Lutumba, mwanamuziki maarufu wa zamani, akiwa pia kiongozi msaidizi wa hayati Lwambo Lwanzo Makiadi Franco, wakiwa na kundi la TP OK Jazz, umeshawasili Kinshasa.

Habari kutoka Congo DR, zinasema kuwa kabla ya kuwasili nchini humo, mwili wa marehemu ulifanyiwa ibada ya kuuaga kwenye Kanisa moja nchini Ufaransa kabla ya kusafirishwa na ndege ya 'Air France' hadi Kinshasa.

Taarifa zinasema, moja kwa moja utapelekwa kuhifadhiwa katika hospitali 'De Cinquantenaire', na baada ya hapo utapelekwa Bungeni kwa ajili ya kuwapa fursa Waheshimiwa kuuga, kabla ya kutipishwa nyumba kwake ili familia, ndugu, jamaa na marafiki kupata fursa ya kuuaga mwili wa mpendwa wao.

Habari kutoka Kinshasa zinaeleza kuwa mbali na kupitishwa huko, pia jeneza lake litapitishwa 'Lutumba Monument', sehemu yenye mnara wa kumbukumbu yake, ili kuwapa nafasi sasa ya wanamuziki wenzake na mashabiki wake wa muziki nao kukusanyika kutoa salamu zao za mwisho.

Kama kawaida kwa Wakongomani, sehemu kama hiyo ndiyo kunakuwa na bendi ambayo hupigwa muziki na nyimbo zote ambazo marehemu alikuwa akizipiga kwenye bendi yake.

Mara nyingi eneo hilo huonekana kana kwamba ni tamasha fulani kubwa, lakini ndiyo sehemu yao ya utamaduni wa kuomboleza msiba, hasa wa wanamuziki wao.


Ni sehemu ambayo kila mmoja huonyesha hisia zake, kwani wapo wanaoimba, kucheza, kugalagala, kulia na kuomboleza pia, huku nyimbo alizotunga, kuimba, au kupiga marehemu zikipigwa laivu na bendi teule inayokuwa jukwaani, ikiwa na wanamuziki wenzake aliowaacha hai.

Mwili wa marehemu Lutumba utalazwa kwenye makazi yake ya milele kwenye makaburi ya 'Nécropole Entre Terre et Ciel', jijini Kinshasa kesho jumapili.

Marehemu alikuwa mtunzi wa nyimbo nyingi za TP OK Jazz na Bana OK iliyoundwa baada ya kifo cha Franco, na chombo alichokuwa akipiga jukwaani ni gitaa la kati la 'rhythm' ambalo alikuwa akilimudu kwa kiwango cha juu.

Moja ya tungo zake ambazo hazitosahaulika ni 'Seydou' na 'Maya'.

Wimbo wa 'Maya', ulitafsiriwa kiswahili hapa nchini na kuimbwa na mwanamuziki Mafumu Bilal. Alifariki akiwa na umri wa miaka 81, huku mwaka jana akistaafu rasmi muziki na gitaa lake kulipeleka Ikulu na Rais Joseph Kabila wakati huo kabla hajaondoka madarakani, kabla ya gitaa hilo kupelekwa Makumbusho ya nchini humo kwa ajili ya kumbukumbu ya vizazi vijavyo.



## Wanamuziki wa 5 waliopigia Msondo, Sikinde





**Na Adam Fungamwango**

KAMA zilivyo Simba na Yanga kwenye soka, kwenye mambo ya muziki nchini kuna utani wa jadi, au upinzani katika bendi mbili kubwa kabisa.

Bendi hizi ni Msondo Ngoma Music Band na Orchestra Mlimani Park, ikitumia mtindo wa Sikinde Ngoma ya Ukae.

Ni bendi zenye mashabiki wengi nchini waliogawanyika pande mbili kama zilivyo timu za mpira wa miguu za Simba na Yanga.

Kila upinzani una historia yake. Msondo ilianzishwa mwaka 1964 na Chama cha Wafanyakazi Tanzania na kuiita NUTA Jazz Band, ikitumia mitindo mbalimbali na baadaye Msondo Ngoma. Ilikuwa ikibadilisha majina ya bendi kulingana na siasa za nchi, hasa Chama Cha Wafanyakazi kilivyokuwa ikijibadisha majina.

Ndiyo maana baadaye ikaitwa JUWATA Jazz Band, OTTU Jazz Band, TFTU Jazz Band na baadaye wanachukua jina la mtindo na Msondo Ngoma ndiyo ikawa jina la band na hii ni baada ya wanamuziki kujitoa kwenye Muungano wa Vyama Vya Wafanyakazi na kujitegemea wenyewe.

Upinzani wao na Sikinde ulianza mwaka 1978, baada ya baadhi ya wanamuziki wa Msondo wakiongozwa na Muhidini Mwalimu Gurumo kwenda kuanzisha Mlimani Park Orchestra.

Hapo ndipo moto ukawaka, kwani kukawa na mashabiki waliohama Msondo na kuwa Sikinde na wengine kubaki kwenye bendi ya awali. Leo tunawaangazia baadhi ya wanamuziki nyota ambao wamewahi kupigia bendi zote mbili hasimu.

### MUHIDINI MWALIMU GURUMO

Alikuwa mmoja wa viongozi wa Juwata Jazz, lakini aliondoka mwaka 1978 na kwenda kuunda Sikinde. Na ni mmoja wa wanamuziki waliosababisha upinzani mkubwa kati ya bendi hizo mbili.

Gurumo ni nembo ya bendi zote hizo mbili kwani hata majina ya Msondo na Sikinde ni yeye ndiye aliyeyabuni.

Hayo ni majina ya ngoma za kwao Uzaramoni. Hata hivyo, Gurumo alirejea tena Msondo mwaka 1990 na hakuhama tena hadi alipofariki 2014 akiwa na miaka 74 na kuzikwa kwao kijiji cha Masaki, Wilayani Kisarawe mkoa wa Pwani.

### HASSAN REHANI BITCHUKA

Alikuwa mwimbaji tegemeo wa sauti ya kwanza kwenye bendi ya Msondo Ngoma.

Hata alipohama Gurumo mwaka 1978, Msondo ilionekana kutotetereka kwa kutoa vibao vingine vikali kama 'Sogea Karibu' na 'Uzuri si Shani'.

Hata hivyo, Sikinde iliwapa pigo Msondo mwaka 1979, ilipomchukua Bitchuka na kuacha kilio kikubwa.

Baada ya miaka 11, Bitchuka alirejea tena Msondo akiwa pamoja na swahiba wake Gurumo, huku wakiwa pia wamepitia bendi ya Orchestra Safari Sound (OSS).

Katikati ya miaka ya 2000, mwimbaji huyo mwenye sauti tamu, aliihama tena Msondo na kurudi Sikinde ambako hadi leo yupo na bendi hiyo.

### SHAABAN DEDE

Baada ya kuhangaika kwa muda mrefu kumpata mtu atakayeweza kufanana sauti na Bitchuka, hatimaye Msondo walimpata mwimbaji wa aina hiyo kutoka Dodoma International, Shaaban Dede.

Huyu alituliza kidogo mizuka ya mashabiki wa Msondo Ngoma kutokana na sauti yake kuwa na mfanano na Bitchuka.

Hiyo ilikuwa mwaka 1979. Lakini kama kawaida ya Sikinde. Huenda ilikuwa ina mikakati ya kuidhoofisha Msondo, kwani mwaka 1982 ilimchukua pia Dede na kuwaacha viongozi na mashabiki wa Msondo wasijue la kufanya.

Alirejea tena Msondo mwishoni mwa miaka ya '80, na kutunga nyimbo kama 'Sauda' na 'Kimwaga' kabla ya kutimuliwa kutokana na kosa la kushindwa kufika kazini na kwenda Uwanja wa Uhuru (zamani Taifa) kutazama mechi ya Simba dhidi ya Sigara. Dede alikuwa ni mwanachana wa klabu ya Simba, kama ilivyo kwa Bitchuka na Gurumo.

Alirejea tena Msondo baada ya kifo cha Tx Moshi William mwaka 2006, hadi na yeye alipofariki Julai 2017.

### FRESH JUMBE

Akitokea Tanga, alichukuliwa na Majirani rajab kwenye bendi ya Dar International, lakini muda mfupi tu akanyakuliwa na Msondo Ngoma. Hiyo ilikuwa ni miaka ya '80.

Akaingia na vibao kama 'Ama Zake Ama zangu' na 'Pamela' zilizompa umaarufu mkubwa. Mwishoni mwa miaka ya '80 alichukuliwa na Sikinde na kutoka na vibao kama 'MV Mapenzi no 2', 'Ramadhani', na nyingine nyingi ambazo aliimba kwa ustadi mkubwa.

Huyu naye anaingia kwenye orodha ya wanamuziki waliowahi kupigia bendi hizo mbili hasimu. Kwa sasa yuko nchini Japan akiendelea na mambo ya muziki.

### SULEIMAN MWANYIRO

Ni mpiga besi ambaye awali alikuwa akipiga kwenye bendi maarufu za taarabu Tanga, Black Star na Lucky Star.

Alichukuliwa na Msondo miaka ya '70 na kufanya kazi kwa umahiri mkubwa hadi alipokuwa mmoja wa wanamuziki walioihama bendi hiyo na kwenda Sikinde.

Naye pia alikuwa mmoja na mlolongo wa wanamuziki waliokuwa wakihama na kurejea tena, kwani miaka ya 2000 alirejea tena Msondo na kutunga vibao vikali kama 'Kauka Nikuvae', 'Sekuntoza Kigudi Chauma', 'Tuelewane Mke wangu' na nyingine nyingi, kabla ya kuelekea tena Sikinde. Alifariki mwaka 2004.



# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**



# Shikolobo: Hakuna kitakachofichika chini ya jua

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA haina siri. Tena waswahili wanaongeza na msemo mwingine kuwa 'na siri si ya watu wawili.'

Siku zote kitu chochote kinachofanywa na binadamu na kutaka kisijulikane kwa watu, huwa anaweza kufanya hivyo kwa siku, mwezi, mwaka au miaka kadhaa. Hata miaka 100 siri inaweza kukaa, lakini haitoweza kukaa milele, ukweli usijulikane.

Mtunzi wa filamu ya 'Shikolobo' amejaribu kuonyesha uhalisia wa jambo hilo. Ni filamu iliyochezwa na wasanii machachari kama Ringo, Tini White, Nass Maburudani, Chimuu, Kipupwe, Hance Popa, Lilly na wengineo.

Inaanza kwa Kipupwe na mwenzake Chimuu wakimkimbiza Ringo akiwa na mapanga mkononi.

Wanamuua na kuchukua mkoba uliokuwa umejaa pesa. Kifo hicho kinaleta simanzi kubwa kijijini hapo hasa kwa mke wa marehemu. Kuanzia hapo akaanza kuishi maisha ya tabu huku akimkumbuka mumewe.

Mpemba akaamua kuchukua jukumu la kumtunza dada yake aliyefiwa na mumewe, ingawa mke alikuwa akiishi kwenye nyumba alioachiwa na marehemu mumewe. Baada ya miezi kadhaa kijijini kikaanza kuwaka moto. Ni taarifa za watu kukutana na mzimu wa Ringo.

Wengine wanadai wamemuona shambani, wengine njiani, ili mradi kila mtu akiongea kwa jinsi alivyomuona.

Hata hivyo kila aliyemuona alikuwa akitimua mbio, hivyo kutokuwa na majibu sahihi ya kile walichokiona.

Hata waliomuua Ringo nao, walikutana na 'mzimu' wake na kutimua mbio, na hii ilisababisha kujutia kitendo chao cha kumuua na kuchukua pesa ambazo tayari walikuwa wameshazimaliza kwa matumizi.

Ukweli ni kwamba haukuwa mzimu wa Ringo. Waliokuwa wanamuona ni pacha wake. Alikuwa wamekuja kijijini hapo kumtafuta ndugu yake kwani hawajaonana tangu walipokuwa wadogo.

Walizaliwa mapacha, lakini wazazi wao walipoachana kila mmoja alimchukua mmoja wao, hivyo Doto aliishi mjini na Kulwa kijijini.

Alipopata taarifa kuwa ndugu yake alipo, alifika kijijini hapo kumtafuta, lakini alikutana na vitimbi kwa kukimbiwa kila alipokutana na mwanakijiji.

Lakini maneno waliyokuwa wanasema, yalimfanya Doto kuhisi kuna kitu, hivyo aliamua kubaki hapo hapo kijijini akizunguka huku na kuko, kuangalia ni nani anaweza kumfumbulia fumbo ya yeye kuogopwa na kukimbiwa.

Hilo linafanikiwa kwani anafanikiwa kuifahamu nyumba ya ndugu yake na pamoja na shemeji yake kumkimbia zaidi ya mara mbili, lakini alimfahamisha kuwa yeye siyo mumewe bali ni pacha wake.

Kwa ujasiri, mke wa marehemu aliamua kumsogelea na kumsikiliza. Ndipo alipohadithiwa ukweli wote na akaamini kuwa mumewe bado ni marehemu na yule aliyekuwepo pale ni ndugu yake.

Doto naye akamuuliza alipo ndugu yake anayemtafuta, akaambiwa kuwa amefariki dunia na ndiyo maana watu wanamkimbia wanapomuona kwa sababu wanadhani ni marehemu amefufuka kwa jinsi walivyofanana.

Kipupwe na Chimuu baada ya tukio la kuona 'mzimu' waliamua 'kuungama', kwenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kwenda kumwambia ukweli wote ili mzimu usiendelee kuwasumbua, lakini kwa sharti la kutoitoa siri hiyo popote pale.

Tini White ambaye ndiye Mwenyekiti, anaahidi kutotoa siri, lakini akawaambia kuwa waingie ndani. Walipoingia aliwafungia kwa nje na kwenda kuiita familia ya marehemu Ringo pamoja na wanakijiji.

Mke wa Ringo, Doto pamoja, shemeji wa marehemu, pamoja baadhi ya wanakijiji walifika kwa Mwenyekiti na kuwakamata Kipupwe na wenzake, kabla ya kuwapeleka mbele ya vyombo vya sheria kwa kosa la mauaji.

# SAUTI ZA WANAMUZIKI WA DRC ZILIZOTIKISA BURUDANI NCHINI


Kassongo Mpinda 'Clyton.'


Tshimanga Kalala Assosa.


Mzee Makassy. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**


Kasaloo Kyanga


Kukumbi Mwanza Mpango - Kingi Kikii.

# WANAOSHIKILIA BURUDANI YA VIJANA



WIDKIZ YOUN



KOREDE



PATORANKING



YEMI



ZAC EFRON

MAKALA

# PADRE DK. MSAFIRI: WANAMAZINGIRA TUTAMUENZI DK. MENGI KWA NJIA KUU TATU



Dk. Reginald Mengi akipanda mti katika ubalozi wa Kenya nchini Tanzania. **PICHA: MAKTABA YETU**

**Na James Lanka, Moshi**

MMOJA wa watu walioguswa na msiba mkubwa wa Mzee Dk. Reginald Mengi, ni Padre, Dk. Aidan Msafiri, Mkurugenzi wa taasisi ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira ya Kilimanjaro Consortium For Development and Environment (KCDE).

Dk. Msafiri, anafafanua hilo akisema: "Ni jambo la Msingi kabisa watu waliofanya mema wakati wa uhai wao hapa duniani kama Dk. Reginald Abraham Mengi, wanapoaga dunia waenziwe kwa namna ambayo haitasahaulika kamwe."

Katika nafasi yake ya kuwa mdau wa mazingira kama alivyokuwa anamtambua Dk. Mengi kuwamo katika watu muhimu waliojitolea maisha yao katika suala la uhifadhi na utunzaji mazingira mkoani Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla.

"Tangu kutangazwa kwa kifo chake mnamo tarehe 2, Mei mwaka huu, wasifu wake umekuwa ukionyeshwa na kusambazwa katika vyombo mbalimbali vya habari, ikiwamo mitandao ya kijamii.

"Ila mimi binafsi ningependa nitoe uchambuzi wangu kuhusu namna tatu za kumuenzi mwanamazingira mwenzetu, Dk. Reginald Abraham Mengi kwa vitendo," anatamka Padre Dk. Msafiri.

Anasema: "Namna hii, kawaida kwa watu mashuhuri na hata watu wa kawaida ya kuandika wasifu, kuweka mashada mazuri ya maua makaburini kuwasha mishumaa wakati wa kuhifadhi miili katika nyumba zake za milele.

"Namna hii husahaulika baada ya muda; lakini namna pekee ya kumuenzi Dk. Mengi ni kuishi maisha ya kuwajali watu wenye mahitaji maalumu kama masikini na walemavu."

Anaendelea kufafanua kuwa, ipo haja kubwa sana ya kumuenzi hayati Dkt Mengi katika maono yake ya kielimu, kiuchumi na utunzaji wa mazingira kwa uchumi endelevu.

Padre, Dk. Msafiri anataja namna nyingine mpya na ya juu zaidi ambayo ni endelevu kwa vizazi vijavyo, ni kujikita katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Namna hii inajikita zaidi katika kuotesha miti ambayo ni mapafu ya yalimwengu," anatamka na kufafanua:

"Ninatoa wito kwa watu na taasisi mbalimbali kuwa, kabla, siku na baada ya mazishi na maziko ya mpendwa wetu na mwanamazingira mwenzetu hodari Dk. Reginald Mengi. Tuoteshe miti ya kivuli, matunda na dawa ambayo ndio mapafu ya dunia."

Dk, Msafiri anaitaja hiyo kuwa njia endelevu na yenye faida kwa vizazi vijavyo kwa Watanzania wote wanaomuenzi, Dk. Mengi, aliyeweka kipaumbele cha utunzaji mazingira kwa kupanda miti ambayo ni mapafu ya dunia.

"Naamini Mungu analo kusudio lake, kwani rafiki yangu Dk. Mengi amefariki katika kipindi ambacho Mungu ameleta baraka ya mvua katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania.

"Hivyo, natoa wito kwa Watanzania wenzangu popote walipo, watumie nafasi hii kwa kumuenzi kwa kupanda miche mbalimbali ya miti ambayo ni rafiki wa mazingira," anasema Dk, Msafiri.

Anafafanua: "Pia, katika sala zetu za kila siku pasipo kujali imani zetu, tumwombe Mungu kwa kusali kwa ajili ya utamaduni wa mpya wa utunzaji wa mazingira.

USHAURI WAKE

"Ninashauri terehe aliyoaga dunia Dk. Mengi (Mei 2), ichukuliwe kama siku maalumu ya kumuenzi kwa kuongeza mapafu ya ulimwengu ambayo ni miti ya aina mbalimbali, kwa kupanda miche mipya ya miti ambayo ni rafiki kwa mazingira."

Padre Dk. Msafiri anatoa wito kwa wasanii mbalimbali wa muziki, kutunga nyimbo za kumuenzi Dk. Reginald katika kuendeleza maono yake katika nyanja za kielimu, kiuchumi, uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

"Natoa wito kwa kila aliyeguswa na kifo cha mwanamazingira nguli, Dk. Reginald Mengi, amuenzi kila anapoadhimisha siku yake ya kuzaliwa (birth day) kwa kupanda idadi ya miti inayolingana na miaka yake.

"Naamini kwa kufanya, hivyo tutakuwa tumeongeza mapafu ya dunia ambayo ni miti pekee," anasisitiza Padre, Dk. Aidan Msafiri, huku akitoa wito wa kujengwa utamaduni wa kutumia zaidi vyakula vya jamii mboga za majani kuliko nyama.

Anatoa ufafanuzi kuwa, kuna manufaa ya kiafya na utunzaji mazingira, kwani uzalishaji wa kilo moja ya nyama hutumia wastani wa maji mara 40 zaidi ya mboga ya majani.

Kwanini uharibifu?

Balozi Dk. Msafiri anasema, ukataji miti ovyo kwa nia ya kupata kuni na mkaa inayotumiwa kama nishati ya kupikia na wananchi wengi hasa wa kipato cha chini na kati umekuwa 'kichocheo' kikubwa katika uharibifu wa mazingira.

Sanjari na hilo, ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa umekuwa chanzo cha mapato kwa wananchi wengi wanaotegemea biashara ya nishati hiyo ya kupikia katika maisha yao ya kila siku, kwa kukata miti ya kuni na mkaa za kuuza.

Pia, anasema kuna tatizo la uvunaji miti pasipo kuzingatia utaratibu maalumu unaozingatia 'ikolojia' ya mimea hasa miti ya asili, umegeuka mwiba kwani tatizo hilo limepelekea baadhi ya maeneo kugeuka 'jangwa' kwa kukosa mvua.

Serikali kupitia wadau mbalimbali wa mazingira ikiwemo taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ikiwemo Wakala wa Misitiu (TFS), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanayojihusisha na uhifadhi wa mazingira na wadau, wamekuwa mstari wa mbele katika kupambana na wananchi wanajihusisha na uharibifu.

Padre, Dk. Msafiri anajitambulisha kuwa Balozi wa Umoja wa Mataifa kuhusu mazingira nchini na ameshirikiana kwa mikakati na kampeni nyingi kuhusu mazingira na upandaji miti mkoani Kilimanjaro na nchini kwa jumla.

● **Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa mawasiliano ya Baruapepe: jlanka6@gmail.com na simu: (+255) 0752 691 129**



Dk. Reginald Mengi akizungumza na wahariri katika moja ya mikutano yao.

# TASNIA YOTE YA HABARI INADONDOSHA MACHOZI

**Na Peter Orwa**

JUZI ni siku iliyobeba tukio zito katika nafsi ya umma wa jamii ya Watanzania na nje ya Tanzania, kuhusiana na habari za kifo cha Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi

Huyo ni mfanyabiashara na mpiganiaji mkubwa wa haki na maendeleo ya umma katika sekta tofauti, hasa aliyewaelekezea jicho walio katika kundi la wanyonge na wanaonuwia kufanikiwa.

Tasia ya habari nayo inabeba majonzi yake pekee, katika nafasi yake kuanzia maudhui kama ya taaluma, ajira, uongozi, biashara, milki ya vyombo vya habari na uendelezaji taaluma.

Binafsi katika msingi wake wa taaluma, Dk. Mengi alibobea katika fani ya uhasibu ambako alikuwa na mchango wa aina nyingi katika fani hiyo.

Hiyo inajumuisha historia kutumikia kazi awali alikoajiriwa tangu mwanzo mwa miaka ya 1970, katika kampuni ya ukaguzi wa hesabu ya Coopers and Lybrand Tanzania, ambayo sasa inajulikana Price Waterhouse Cooper.

Pia, alishawahi kuwamo katika uongozi wa bodi inayosimamia Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), ambayo jukumu lake kuu ni kusimamia taaluma ya uhasibu.

Lakini, katika mustakabali mpana, tafsiri yake kitaaluma ilivuka uhasibu na badala yake ilibeba sura pana ya sekta ya biashara, ambayo hasa ndiyo ailonyesha uwezo wake kwa vitendo muda mrefu, hadi safari yake ya mwisho duniani wiki hii, ambayo umma wote bado unahuzunika.

Katika tasnia ya habari ambako nako aliendeleza biashara kama ilivyo baadhi ya sekta nyinginezo. Ni mwanzoni mwa miaka ya 1990, Tanzania mara tu baada ya serikali kufungua milango ya kuanzisha ulingo huria katika sekta ya habari ilileta changamoto kubwa.

Ikumbukwe katika za mageuzi, sekta nyingi zilifanyiwa mabadiliko katika kipindi hicho kuidhinisha uhuria wa shuguili nyingi, mathalani uhuria wa kisiasa na benki katika zama hizo kati ya mwaka 1991 na 1993, vivyo hivyo uhuria ukaonekana katika vyombo vya habari.

IPP imo katika orodha ya waasisi hao walioanza kwa kishindo ndani ya soko jipya la habari. Hapo zinatajwa kampuni za Redio One na televisheni ya ITV, zilizofungua mlango huria wa mawasiliano.

Redio na televisheni hizo kuanzia zama hizo za mwaka 1993 hadi 1994 ikijiimarisha zaidi, IPP ilipanua zaidi wigo kwa kuanzisha rasmi, magazeti yake kama The Guardian, Sunday Observer na Nipashe.

Hicho kilikuwa kipindi kifupi kutoka zama za kuanza kuchapishwa sokoni magazeti mawili binafsi huria wa habari.

ITV ina sifa yake nyingine ya ziada, kwamba imedumu kuwa televisheni ya kwanza kushuhudiwa na Watanzania katika mazingira huria ya mawasiliano ya umma, ikibeba moto wa ufanisi uliokuwa wa kipekee.

Ni hadhi ya chombo inayoendelezwa, kwa kushikilia tuzo ya kimataifa, ukiwa ni ujumbe kwamba 'taa uliyowashwa na Dk. Mengi haijazimika.'

Baadaye, kama zilivyo radio na televisheni za East African (EATV) na Capital zilivyoanzishwa, ndivyo katika sura nyingineyo kwenye gazeti ziliongezeka nyingi, kama vile Alasiri, Kasheshe, Taifa Letu, Financial Times, Lete Raha, Kulikoni na This Day

Kuna mambo kadhaa yanayoendana na kuanzishwa vyombo vya habari vya IPP ambavyo vilichangia kupanua ghafla fursa ya ajira nchini katika sekta hiyo kwa kuzingatia usomaji na usikivu wake uliotawala kwa mapana.

Sehemu mojawapo ya manufaa hayo, ni magazeti na usikivu wa redio na televisheni kufika mbali sana kila upande wa nchi.

Ni hali iliyoenda sambamba na kukua kwa ushindani wa soko la bidhaa zenyewe za habari ufanisi ukatanuka, katika mfumo magazeti na usikilizaji wa kielektroniki unaboreshehwa kila uchao.

Kumbukumbu nyingine inayopatikana katika nyayo za Dk. Mengi, ni namna vyombo hivyo vilivyoanza vikiwa na nyenzo bora za utendaji, zikiwamo magari mapya aina ya Maruti, kamera za kisasa kwa wanahabari, ofisi nchini kote na mengineyo kuhudumia watendaji wake waliokuwapo kazini, Dar ea Salaam, na nje ya jiji hilo.

Ni katika zama ambazo Mwenyekiti Mtendaji huyo wa IPP katika siku za awali, alibuni mfumo wa kuwa na ushirika wa kimenjmenti na uongozi, pia wataalamu wa magazeti hayo akikutana nao kufanya tathmini walau kila wiki.

Vyombo vya redio za kielektroiniki, bado vinaendelea kuwa marejeo katika vipindi vya kuigwa vya radio za Fm, ambavyo vimedumu kutawala mvuto wa umma, katika mahitaji ya kijamii katika kipindi husika.

Ni historia inayochukua sura ya robo karne sasa, kwamba sehemu kubwa na majina makubwa kwa madogo ya wanahabari yana 'nyayo' za kuwahi kupitia vyombo vya IPP.

Haikutosha, Dk. Mengi binafsi amekuwa rafiki na mdau wa karibu wa wanahabari na vyombo vyao katika namna mbalimbal, mfano hai ni kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT).

Aidha, aliviunga mkono vyama vyao vya kitaaluma na wanahabari binfasi kila mara kwa mawazo, hata vitendo.

Aliwafahamu wanahabari, nao walifahamu kwa karibu kutokana na ujirani aliyojiweka nao.

Hata maisha ya ushirikiano wao ukagusa misaada kama anayoifanya kwa jumuiya nyinginezo zilizopo.

Edda Sanga, ni mwanahabari aliyetangaza Radio Tanzania kwa muda mrefu, pia baadaye kutumikia vyombo vingine kama vile Radio Mlimani na kuongoza Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa), anakiri mchango mkubwa wa Dk. Mengi kuinua nafasi yao kitaaluma.

Edda akizungumza juzi usiku katika televisheni alipohojiwa, anasema walipotumikia Radio Tanzania (RTD), Dk. Mengi alichangia mengi katika kuwashauri kitaaluma na kuwasaidia kuinuka katika ufanisi kwa kazi.

Ni namna gani, wanahabari wanaweza kulieleza hilo? Ni sentensi moja ya kukiri 'Ni Pigo Kubwa' ndio inayoweza kubeba picha ya maumivu na hasara iliyopata, akibeba sura ya kuwa mzazi wao.

# Wanahabari kuuawa duniani bado janga linalowaelemea

## ■Ya Jamal Khashoggi bado alama
## ■Walia Marekani hakuwafai kikazi



Mwanahabari, Jamal Kashoggi.

**Na Mwandishi Wetu**

TAKRIBAN waandishi wa habari 95, wameuawa mwaka jana wakiwa kazini, kwa mujibu wa Shirikisho la Waandishi Habari wa Kimataifa (IFJ).

Idadi hiyo inatajwa kuwa juu zaidi ya iliyoshuhudiwa mwaka 2017. Hata hivyo, inaelezwa kiwango kupungua, kulinganisha na vilivyoshuhudiwa katika miaka ya nyuma wakati mzozo katika mataifa ya Irak na Syria yalipokuwa yako juu.

Kiwango kikubwa cha vifo vya waandishi habari kilichowahi kunukuliwa ni waandishi 155 mnamo mwaka 2006.

Kifo cha mwandishi kilichogusa dunia mwaka jana, ni cha mwanahabari wa Saudia Jamal Khashoggi, aliyeuawa mnamo mwezi Oktoba, baada ya kwenda katika ubalozi wa Saudia nchini Uturuki.

Mkasa huo ulizusha mzozo wa kidiplomasia kati ya mataifa hayo mawili na shutuma kali za kimataifa.

Pia, kuna mkasa wa mwandishi wa habari za kiuchunguzi wa nchini Ghana, aliyepigwa risasi hadi kufa wakati akiendesha gari kwenda nyumbani, ikielezwa aliuawa kwa kisa cha mwanasiasa dhidi yake.

Vyombo vya habari vya ndani nchini humo, viliripoti kuwa watu wasiojulikana wakiwa katika pikipiki walimpiga risasi Ahmed Hussein-Suale mara tatu katika mji mkuu wa Accra.

Alikuwa miongoni mwa wahusika wa shirika binafsi la upelelezi Tiger Eye na anaelezwa alifuatilia rushwa katika ligi ya mpira wa miguu nchini Ghana.

Wapi hatari zaidi?

Afghanistan inasalia kuwa nchi ilio hatari zaidi kuishi kama mwandishi habari, kukishuhudiwa vifo vya waandishi 16 mwaka jana.

Waandishi tisa walifariki kwa wakati mmoja nchini Afghanistan katika mji mkuu Kabul, baada ya kufika katika eneo la shambulio la bomu kuripoti kuhusu kilichotokea.

Kumelipuliwa bomu la pili na mlipuaji aliyesemekana kujifanya kuwa mwandishi habari.

Katika eneo la Mashariki mwa Afghanistan, mwandishi wa Shirika na Utangazaji la Uingereza (BBC), Ahmad Shah, aliuawa katika moja ya mashambulio hayo katika jimbo la Khost.

Pia, Marekani waandishi habari walifariki mwaka jana. Watano walipigwa risasi katika shambulio dhidi ya ofisi za gazeti la Capital Gazette huko jimbo la Maryland, lililotekelezwa na mwanamume anayearifiwa alijaribu kulishtaki gazeti hilo miaka kadhaa nyuma.

Kutoweza kuvumilia taarifa za habari zinazochapishwa, umaarufu, pamoja na rushwa na uhalifu ni vigezo muhimu sasa linasema IFJ.

"Mazingira ambayo kuna waandishi zaidi wa habari wanauawa kwa kuangazia masaibu kwa jamii zao, mijini na hata mataifa, kuliko kuripoti matukio katika maeneo yanayokumbwa na mizozo," inasema IFJ.

**WAANDISHI WALIOFUNGWA**

Kamati ya Kuwalinda Waandishi Habari (CPJ) huwapiga picha waandishi wa habari waliofungwa gerezani mwanzo wa mwezi Desemba kila mwaka.

Takwimu hizo hujumuisha yeyote anayefanya kazi kama mwandishi habari, aliyefungwa kwa shughuli zinazohusiana na kazi yake.

Mataifa yenye idadi kubwa ya waandishi waliofungwa mnamo 2018 ni pamoja na: Uturuki (68); China 47; Misri (25); Saudi Arabia na Eritrea, 16 kila moja

Uandishi wa demokrasia

Umoja wa Mataifa mwaka huu, unaangazia jukumu kuu la uandishi huru wa habari, kwa demokrasia, hususan wakati wa uchaguzi.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anasema katika taarifa yake kwamba "hakuna demokrasia iliokamilika pasi kuwapo habari za wazi na za kuaminika."

Courtney Radsch, kutoka kamati ya kuwalinda waandishi habari CPJ, anasema kauli za kupinga uandishi habari zimeongezeka katika nchi nyingi akitaja zaidi nchi za Ufilipino na Marekani.

Anaamini kuwa, mitandao ya kijamii na intaneti kwa jumla zimechangia katika masaibu yanayowakabili waandishi habari duniani.

Katika taarifa za mwaka huu katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, kundi la waandishi wasio na mipaka (RSF) wanaitaja hali Marekani kuwa ni 'tatizo'.

Marekani imeshuka kwenye orodha ya RSF katika uhuru wa waandishi habari mwaka huu na kama ilivyo kwa India na Brazil.

Lakini RSF inaongeza kwamba, mataifa yaliyoshuhudia kiwango kibaya cha uhuru wa vyombo vya habari, ni pamoja na Venezuela, Russia na China, ambazo zimezidi kudidimia chini mwaka huu.

**BBC**



Waandishi wa habari wa Marekani wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

# Shida ya maji inavyokwamisha Kilimo kwa kinamama Korogwe

## ▪Ndoo vichwani imeshika muda wa jembe

Na Jenifer Julius

ESTER Jeremia, ni mkazi wa kijiji cha kilole, kata ya Kwamgumi, katika Halmashauri ya mji wa Korogwe.

Ni mmoja kati ya wanawake 2,655 wanaoishi katika kijiji hicho, kinachosifika kwa kilimo cha biashara cha mpunga na mahindi.

Mama huyu huamka saa 11.00 asubuhi kuwahi shambani kulima na kisha anarudi nyumbani mapema, huku akimwacha mume wake akiendelea kuandaa mashamba yao.

Anaelezea sababu ya kuondoka mapema kwamba :"Inanibidi nitoke shamba mapema, ili niwahi kuchota maji ya mifugo na matumizi ya nyumbani kabla jua halijawa kali kwa kuwa maji yanapatikana mbali.

"Kutoka huku Kilole Mzee ninapoishi hadi Ruvu maji yanakopatikana ni mbali. Ninatumia takribani saa mbili kuchota ndoo nane,"

Anasema, kitendo cha kumwacha mume wake shambani, kinapunguza nguvukazi, hali inayosababisha wakati mwingine asifikie malengo yao.

"Kwa kawaida tunalima ekari mbili, ila mwaka jana tumelima ekari moja tu. Mvua imetukuta katikati ikatubidi tuanze kupanda. Hivyo, ekari nzima hatujalima, tumepata hela ya mtaji tuna tuna watoto wanatutegemea," analalamika Ester.

Kimsingi, si mama huyo peke yake anayekumbwa na adha ya shida ya maji katika kijiji hicho.

Yupo Adavent Kibona, mwalimu wa sekondari ya Nyerere, anayeangukia katika adha hiyo. Anasema licha ya kuwapo bomba la maji kijijini hapo, bado halikidhi mahitaji yao kwa kuwa lipo moja tu katika kata nzima ambayo ina watu wakazi wengi .

Mama huyo mwenye mume na watoto wanne, analazimika kuingia bajeti ya kutumia Sh. 2000 kila siku kununua ndoo 10 za maji ya kutoka Mto Ruvu na Sh. 1000 ya kununua maji ya bomba ambayo anatumia kunywa na kupikia.

"Shilingi 3000 kwa siku ni hela nyingi dada, ukitegemea mimi ni mtumishi, mshahara wenyewe ni mdogo, ila nalazimika kununua kwani sina muda wa kwenda kuchota maji na watoto ni wadogo" analalamika Advert.

Asha Hiso, ni mwingine anayeangukia kundi hilo, analazimika kupikia maji ya Mto Ruvu kwa kuwa, hana uwezo wa kununua maji ya bomba kila siku.

"Maji ya bomba yanauzwa dumu shilingi 500. Sina uwezo wa kununua madumu mengi, hivyo tunapikia haya haya ya Ruvu. Huwa nanunua dumu moja la maji ya kunywa kila baada ya siku mbili," anaeleza maisha yake.



Ester Jeremia akichota maji pamoja na wanawake wengine katika kijiji cha Kilole.



Mkazi wa kijiji cha Kilole akifua nguo katika Mto Ruvu. **PICHA: JENIFER JULIUS**

Shida ya maji katika kijiji hicho ni tofauti na vitongoji jirani vya mji wa Korogwe, kama vile Manundu na Old Korogwe, ambavyo katika wastani wa kila nyumba tano, moja ina bomba linalotoa maji safi.

Kijoli Khallage, mkazi wa Old Korogwe, anasema licha ya Mto Ruvu kupita katika eneo hilo lakini hawayatumii kwa kuwa wana mabomba ya nayotoa maji safi .

"Sijawahi kwenda kuchota maji Mto Ruvu. Tuna mabomba ya kutosha yanayotoa majisafi. Hata hao wanaokwenda (mto)Ruvu mara nyingi ni kwa ajili ya kufua tu na labda itokee maji yamekatika," anafafanua Kijoli.

**MWENYEKITI S/MTAA**

Mathew Msanga, ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kwamgumi, anayekiri kuwa wanawake wa kijiji hiki kimebebwa na wanawake, wenzetu hawa wanatuongoza kwa kila kitu, mfano mdogo tu katika wakulima 165 waliojiandikisha 88 ni wanawake na wanalima kila mwaka".

Anaeleza kuwa serikali inatambua kero hiyo na mikakati ya kuleta maji kijijini hapo imeshaanza, kwa mwaka juzi walifika wataalamu waliopima ramani kwa ajili ya kuchimba mitaro ya kupitishia mabomba.

"Mikakati ya kuleta maji imeshaanza. Awamu ya upimaji ramani imeshafanyika mwaka juzi, hivyo tunaisubiri awamu ya pili. Natumai ni tatizo hili litaisha na tutamtua ndoo mwanamke muda si mrefu,"anamalizia Methew.

**DED**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri wa Mji wa Korogwe, Jumanne Shauri, anasema kuna changamoto ya maji katika halmashauri hasa kata ya Kwamngumi, lakini wameshaanza kuifanyia kazi.

Anasema wamesaini mkataba na shirika la Kijerumani la GIZ, kwa ajili ya kujenga mabomba na kusambaza maji na kuhakikisha kila kaya ina choo salama.

"Tumeshasaini mkataba na shirika la GIZ na hatua za kwanza za mradi zimeshaanza, kwa kuhamasisha kila kaya kujenga choo bora na kupima ramani imeshafanyika," anasema

Katika hatua ya pili ya mradi huo, Shauri anasema watachimba mitaro na kuweka mabomba katika vijiji vya Manzese, Kilole na kisha Kwamngumi.

Ikirejewa, Sera yaTaifa ya Maji ya Mwaka 2002, maelekezo ni kuwapatia wananchi wote waishio vijijini wanapaswa kupata huduma ya maji safi na salama, katika umbali usiozidi mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

Katika kutimiza hilo, serikali inalenga kufikia asilimia 85 ya wananchi wanaopata maji safi na salama katika maeneo ya vijijini, ifikapo mwaka 2020.

## HABARI KIMATAIFA

# Bobi wine aachiwa kwa dhamana

**KAMPALA,** Uganda

MSANII na mwanasiasa wa upinzani Uganda, Robert Kyagulanyi (Bobi Wine), ameachiwa kwa dhamana na mahakama mjini Kampala.

Mchakato wa kusikiliza ombi lake la dhamana uliendeshwa kwa njia ya video akiwa gerezani Luzira.

Bobi wine aliweza kuwasiliana na hakimu kupitia mawasiliano hayo ya video, hatua iliyoepusha kutokea kwa vurugu endapo angesafirishwa hadi mahakamani.

Wine alishtakiwa kwa kosa la kushiriki katika maandamano ambayo hayakupata kibali cha polisi mwaka jana, pamoja na kupinga kodi ya kutumia mitandao ya kijamii maarufu Uganda kama OTT.

Wafuasi wa mbunge huyo walionekana wakiimba wimbo wao wa ushindi baada ya hakimu wa mahakama ya Buganda Road kukubali ombi la Bobi Wine kupewa dhamana.

**Wanataka Bobi wine asiwe huru nchini mwetu, Kwa sababu polisi wanaweza kukamata watu bila mpango, wanaweza kukukamata ukiwa unafanya kazi yako unaenda kula, wanakukamata.**

Uamuzi wa Wine kupewa dhamana ulitolewa katika kikao kilichochukua muda wa saa nne, upande wa serikali ukipinga apewe dhamana.

Kabla ya hakimu kumpatia dhamana, Bobi Wine alipewa nafasi ya kuzungumuza ambapo alisema: "Napenda kusisitiza kwamba sio mimi ninayeshitakiwa mahakamani, maamuzi ya mahakama yatakayotolewa sio tatizo kwangu, mimi nitaendelea kusema ukweli".

"Kazi yangu ni kutetea haki, kazi yangu ni kupigania haki yako wewe hakimu na mimi na raia wengine wa Uganda. Kama itakuwa haki mimi kubaki hapa korokoroni, nitamshukuru mwenyezi Mungu kwa sababu nina kazi nyingi za kufanya hata hapa gerezani' alisema mwanasiasa huyo.

Wine alipewa masharti magumu ya dhamana kulingana na umarufu wake anapopita mjini, ambapo huwa anaambatana na wafuasi wengi.

Wakili wa mwanasiasa huyo, Asumani Basalilwa alisema mojawapo ya sharti alilopewa mteja wake ni kutohusika katika mkusanyiko au maandamano.

"Haya masharti yanashangaza kwa sababu ni nani ana uwezo wa kusema maandamano ni mazuri au mabaya? Wanataka Bobi wine asiwe huru nchini mwetu, Kwa sababu polisi wanaweza kukamata watu bila mpango, wanaweza kukukamata ukiwa unafanya kazi yako unaenda kula, wanakukamata. Kama ni mahakama itasema mkutano huu ni haramu, hivyo ni vizuri lakini kama ni polisi, kutakuwa na vita vingi," alisema wakili Asumani.

Licha ya masharti aliyopewa, mawakili wake hawakufurahishwa na mfumo wa mahakama uliotumiwa wa teknolojia bila ya kuwasiliana na mteja wao akiwa Luzira.

"Sio teknolojia mbaya, lakini leo sheria yetu Uganda inasema, ni lazima uje mahakamani uwasilishe ombi kama unataka kufanya video conference. Lakini hakuna aliyekuja hapa kuwasilisha ombi hilo, kwa hivyo kilichofanyika hapa ni kinyume cha sheria," alisema wakili Asumani.

Alisema watu waliokuwapo mahakamani hawakufurahishwa na maamuzi ya mahakama jinsi serikali inavyomnyima haki za kufanya kazi Kyagulanyi.

Kampeni mpya ilianzishwa katika mitandao ya kutaka Bobi Wine aachiliwe huru.

Mashirika ya kutetea haki za binaadamu likiwamo la Tom Lantos Human Rights Commission la Marekani, Shirika linaloshinikiza uongozi wenye maadili na demokrasia kwa wote - Vanguard Africa, yameshutumu hatua hiyo ya serikali ya Uganda.

Bobi Wine alikamatwa siku ya Jumatatu wakati akilipokuwa njiani kupeleka barua makao makuu ya polisi kuwafahamisha anakwenda kufanya maandamano ya kuminywa haki zake za kufanya kazi zake za muziki. **BBC**

## Maduro awahimiza wanajeshi kupambana na wasaliti

**CARCAS,** Venezuela

RAIS wa Venezuela, Nicolas Maduro amelitaka jeshi la nchi hiyo kumkabili yeyote anayepanga njama ya mapinduzi, baada ya uasi wa wanajeshi wanaomuunga mkono kiongozi wa upinzani, Juan Guaido kuzimwa.

Akizungumza katika hafla iliyohudhuriwa na wanajeshi 4,500, Rais Maduro alisema kuwa hakuna anayeweza kuwa muoga kwa sababu ni wakati wa kuilinda amani ya nchi.

Waziri wa Ulinzi, Vladmir Padrino, alisema wanajeshi walikusanyika kuonyesha utiifu wao kwa Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye Rais Nicolas Maduro.

Guaido ambaye anatambuliwa na zaidi ya nchi 50 kuwa rais wa mpito wa nchi hiyo iliyogubikwa na mzozo, aliwaomba wanajeshi kumuondoa madarakani kiongozi huyo anayekabiliwa na shinikizo.

Kundi dogo liliitikia wito huo, lakini vuguvugu hilo likashindwa, ambapo uongozi wa kijeshi umetangaza kuiunga mkono serikali iliyopo madarakani inayoongozwa na Rais Maduro.

Wakati huo huo, mahakama ya juu ya Venezuela iliamuru kukamatwa tena kwa kiongozi wa upinzani mwenye ushawishi, Leopoldo Lopez ambaye alijitokeza kwa pamoja na Guaido baada ya kutoroshwa kutoka kifungo cha nyumbani.

Mpaka sasa, wanajeshi waasi 25 wamechukua hifadhi katika ubalozi wa Brazil.

Akizungumza katika makazi ya balozi wa Hispania, Lopez mwenye umri wa miaka 48 alisema uasi mdogo uliofanywa utaufikisha kikomo udikteta wa Rais Maduro. **DW**




Waandishi wa habari wakionesha ishara ya ukiukwaji na uminywaji wa uhuru wa vyombo vya habari katika mataifa mengi duniani. **PICHA: AFP**

## Waandishi waliofungwa watunukiwa

**NAYPYIDAW,** Myanmar

WAKATI jana ikiwani Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, Umoja wa Mataifa (UN) imetumia siku hiyo kuwatunuku waandishi wa habari wawili tuzo ya juu ya uhuru wa vyombo vya habari.

Waandishi hao Wa Lone na Kyaw Soe wanatoka Shirika la habari la Reuters ambao wanatumikia kifungo cha miaka saba nchini Myanmar.

Walitunukiwa tuzo hiyo katika mkesha wa maadhimisho ya siku hiyo ambayo mwaka huu kitaifa yamefanyika Ethiopia.

Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la UN (UNESCO) liliikabidhi Tuzo ya Uhuru wa Habari ya Guillermo Cano kwa Thura Aung, kaka yake Wa Lone, wakati wa sherehe hizo mjini Addis Ababa. ]

Waandishi hao wawili walikamatwa mwishoni mwa mwaka 2017 wakati wakichunguza operesheni ya kijeshi na uvunjaji wa haki za binaadamu, yakiwamo mauaji ya kiholela, nchini Myanmar. Baadaye waandishi hao walitiwa hatiani kwa kuvunja Sheria ya Siri za Serikali.

UN na makundi mengine ya haki za binaadamu wamekuwa wakiishutumu serikali ya Myanmar kwa kuendesha kampeni ya kuwaangamiza Waislamu wa jamii ya Rohingya. **DW**

## May amtumbua Waziri wa Ulinzi

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Theresa May, juzi alimfuta kazi waziri wake wa ulinzi, Gavin Williamson akisema kwamba amepata ushahidi kuwa alihusika katika kuirahisishia kampuni ya masiliano ya China Huawei kufanya udukuzi kwenye teknolojia ya Uingereza ya mtandao wa mawasiliano wa G5.

Kufutwa kazi kwa Williamson kumechochewa haswa na ripoti iliyochapishwa mwezi Aprili na gazeti moja la Uingereza likisema kwamba waziri huyo aliiruhusu kampuni ya Huawei kuingia kwenye mtandao huo wa G5 katika mkutano wa usalama wa kitaifa.

Lakini Williamson alikanusha madai hayo alipoulizwa na wanahabari. Uingereza ambaye ni mshirika mkuu wa Marekani, imekuwa ikapata shinikizo la Marekani kuitenga kabisa Huawei kwenye mtandao huo wa G5 kwa hofu kwamba kampuni hiyo inaweza kutumia teknolojia hiyo kwa kuifanyia ujasusi serikali ya China. **VOA**

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kujeruhiwa. Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia, ni ajali iliyopangwa na muuaji , mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki

# KISANDUKU CHEUSI - 46

**Na Adam Fungamwango**

NDANI ya hoteli ya Cassanova kulikuwa na watu wengi. Wengine walikuwa wakipata vinywaji taratibu. Wengine walikuwa wakicheza muziki sehemu ambayo ilitengwa kwa ajili hiyo tu.

Siku hiyo hoteli ilipokea wateja wawili wapya, mbali na wale ambao siku zote wamekuwa wenyeji sehemu hiyo.

Walikuwa wamekaa kwenye viti vilivyokuwa kwenye kona ya pembeni inayotazama mlango mkuu.

Hao ni Eddy na Lilly. Tayari Lilly alikuwa ameshakunywa bila kadhaa ambazo zilimfanya kulala kwenye mapaja ya Eddy.

Kwa upande wake hakuna mnywaji sana. Mpaka wakati ule alikuwa ameshakunywa bia mbili tu. Na alikuwa na mpango wa kuagiza ya tatu amalize kazi.

Na huwa anakunywa kwa ajili ya kampani tu, kwa kawaida hakuwa yule mtu ambaye kila siku yuko baa.

Utakapomuona mara kwa mara yuko baa au kwenye mahoteli si kwa ajili ya kunywa, bali kwa ajili ya kazi yake.

Mara taarifa ya habari kwenye televisheni bora kabisa nchini ya ITV ikaanza kuonyeshwa.

"Polisi nchini wamemkamata Mkurugenzi na mmiliki wa hoteli ya Paradiso Benson Mapunda na wenzake kwa tuhuma za kulipua basi la abiria, liitwalo Bomoa Trans na kuua zaidi ya watu 10 na kujeruhi zaidi ya watu 20.

Ajali hiyo ilitokea miezi sita iliyopita eneo la Mikese mkoani Morogoro wakati basi hilo lilipokuwa likitokea Dar es Salaam kwenda Ifakara mkoani humo.

Taarifa zinasema kuwa basi hilo halikuungua moto kutokana na hitilafu ya injini kama ilivyodaiwa kwenye uchunguzi wa awali, bali lililipuliwa kwa bomu lililokuwa limebebwa na mmoja wa abiria ndani ya basi hilo, lilokuwa ameliweka kwenye kisanduku cheusi 'breafcase'."

Wakati huo Kamanda wa Polisi Mkoa alionekana akiongea na Watanzania akiwahabarisha yote yaliyotokea, huku akionyesha watuhumiwa wote waliokuwa wamekamatwa, akiongozwa na Mapunda.

"Taarifa ya habari iliendelea. " Inadaiwa Mapunda alimtuma mmoja wa wasaidizi wake ambaye baada ya kufika eneo hilo alimuomba dereva kwenda kujisaidia, lakini aliiacha 'breafcase' ndani ya basi na alipotoka, dakika mbili tu baadaye mlipuko mkubwa ulitokea na basi kuteketea, huku msaidizi huyo na abiria wachache waliokuwa nao wameteremka kujisaidia wakinusurika."

"Mtuhumiwa pia kwa kutumia wasaidizi au wafanyakazi wake, aliwaua watu wengine wawili waliojulikana kwa majina Hellen na Said kwa nyakati tofauti kwa ajili ya kulinda siri ya mauaji hayo.

Ushahidi awali unaonyesha kuwa mtuhumiwa namba moja Mapunda alifanya kitendo hicho ikiwa ni kulipa kisasi kwa aliyekuwa mchumba wake Careen.

Inasemekana kuwa Mapunda na Careen walikuwa wapenzi, lakini baada ya kuona hakuna ndoa, Careen aliamua kumucha mpenzi wake na kuchumbiwa na mwanaume mwingine aitwaye Peter Mayambua ambaye pia ni marehemu na alijiua kwa uchungu baada ya mpenzi wake kufa.

Taarifa zinaendelea kusema kuwa baada ya kusikia hivyo, Mapunda alihakikisha ndoa hiyo haifanikiwi na haifungwi na alichofanya ni kumuua mpenzi wake Careen kwa kulipua basi hilo alilokuwa amepanda kwenda Ifaraka kwenye ndoa yake.

Tayari inasemekana mipango ya harusi ilikuwa imeshafanywa na Careen alikuwa anakwenda kujiandaa na ndoa, hivyo Mapunda alichofanya ni kuhakikisha anakatisha maisha yake kabla hajafunga ndoa na alitumia njia hiyo ambayo aliona si rahisi kwa vyombo vya usalama kujua.

Ni yule yule kijana mzalendo, Eddy Kamal aliyebaini mpango huo mchafu, akapelelelezа kama ilivyo kawaida yake na kuibuka na kila kitu kilichojificha juu ya mpango mzima wa tukio hilo.

**Taarifa zinaendelea kusema kuwa baada ya kusikia hivyo, Mapunda alihakikisha ndoa hiyo haifanikiwi na haifungwi na alichofanya ni kumuua mpenzi wake Careen kwa kulipua basi hilo alilokuwa amepanda kwenda Ifaraka kwenye ndoa yake.**

Kwa sasa mtuhumiwa na wenzake wapo kizuizini, wengine wakiwa wameuawa kwa mpambano na kijana Eddy aliye chini ya Idara ya Usalama, na sasa mambo yote yapo chini ya polisi na wanatarajiwa kufikishwa Mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili," Ilimaliza taarifa hiyo iliyokuwa imewafanya hata waliokuwa wamelewa chakari kuifutilia kwa makini.

"Du huyu Eddy kiboko, yaani kila tukio tata ujue yumo." Alisikika mtu mmoja liyekuwa karibu na meza ya Lilly na Eddy.

Wengi walionyesha kushangaa na kusikitika kwa wakati mmoja.

"Yaani demu anakukataa wewe unamuua? Si unatafuta mwingine? Wanawake wote hawa Bongo hapa bado unafanya mchezo wa kitoto, ona sasa umekamatwa." Alisikika mtu mmoja ambaye sauti yake tu ilionyesha kuwa alihitaji kurudishwa nyumbani wakati ule kwa kuzidiwa na kilevi.

"Basi wewe hujasikia vizuri, siyo hivyo?" Mwenzie alimbishia.

"Yaani wewe ndiyo umesikia vizuri kuliko mimi?" Alimuuliza kwa dharau.

"Ndiyo wewe umelewa bwana ndiyo maana hujasikia vizuri"

"Haya nieleze wewe mwenzangu ambaye ulikuwa unakunywa soda, hunywi bia kama mimi." Aliuliza kwa kumkoga kwani wote hao walikuwa wakinywa bia.

"Yule demu siyo kama alimkataa huyo jamaa, sema alikuwa hamuoi, anamchezea tu miaka inazidi kwenda, ndiyo akaona bora kaolewe na mwingine, jamaa ndiyo akafanya mambo yake." Jamaa alimfafanulia mwenzake na alikuwa yuko sahihi zaidi.

"Aaah sasa si yale yale tu kama nilivyosema mimi, ila sema wewe umepambanua tu." Mwenzake hakukubali kushindwa.

Kwa bahati nzuri alionyeshwa Kamanda na watuhumiwa, lakini hakuna hata sehemu ambayo alionyesha Eddy au picha yake tu.

Hata siku moja hakutaka picha yake ichapishwe kwenye gazeti au kuonyesha kwenye televisheni kwa sababu ya usalama.

Kutojulikana kwake sura ndiyo kunafanya iwe rahisi kwake kuendelea kufanya kazi kama hizi kwa ufanisi zaidi.

Na ndiyo maana hakuna hata mmoja kwenye hoteli hiyo aliyejua kuwa yule mtu shujaa anayeimbwa na kusifiwa na Watanzania wengi yumo mle ndani.

Mwenyewe alikuwa na furaha kubwa baada ya kumaliza kazi kubwa iliyokuwa inamkabili.

Hata hivyo, moyo bado ulikuwa unamuuma kwa kumpoteza Hellen, msichana aliyetokea kumpenda kwa kipindi kifupi tu tangu walipokutana.

Akakumbuka kuwa ni yeye ndiye aliyesababisha kifo cha Msichana Hellen, pacha wa Careen ambaye aliuawa baada ya kuonekana anataka kutoa siri ya kifo cha ndugu yake kwake. Na hilo ndilo lililomsukuma hadi kuingia kwenye mkasa huu kutafuta siri ya kifo cha Hellen na kukutana na madudu ya Mapunda na marafiki zake.

"Vipi mbona uko kimya muda mrefu." Alizinduliwa na sauti ya Lilly.

"Nilikuwa nawasikiliza hawa jamaa waliokuwa anabishana."

"Maana naona kama vile kuna kitu unawaza."

"Usiwe na wasiwasi mama lwo nipo kwa ajili yako, tukitoka hapa tunaenda nyumbani kwangu."

Lilly alitabasamu na hakuamini maneno ya Eddy kwani mara nyingi huwa wanamuahidi kumtoa 'auti', lakini wapi, ila kwa mara ya kwanza leo anajikuta amepata bahati hiyo.

Kama mwanamke mwingine yoyote, Lilly alikuwa akiona wivu wasichana warembo wa kila aina wakija kwenye ofisi ya bosi wake na yeye akiwa sekretari wake akiwapokea. Pia barua pepe mbalimbali zilikuwa zikimiminika, zingine zikiwa na kikazi zingine zikimtaka kimapenzi kutokana na umaarufu tu aliokuwa nayo kwa ajili ya kazi yake.

"Sisi wengine vinyago vya mpapure hatuwezi kutolewa 'auti' hata siku moja." Siku moja alimpasha Eddy.

"Siku nitakayokutoa 'auti' ndiyo nitakuonyesha kama wewe ni mwanamke wa aina gani, jiamini tu." alimjibu.

"Haya sasa leo ndiyo siku yako ya kutamba Lilly, 'auti' nimekutoa, sasa nini tena unahitaji, kesho sitaki lawama na mtu."

"Leo Samaki unaye mwenyewe Eddy, sasa utajua mwenyewe kama kumkaanga au kumla mbichi." Wote waliangua kicheko, wakakumbatiana.

*mwisho*



TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## CHETI KIMEPOTEA



115211602

**Albert J. Gama** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0751-0031** namba ya cheti **CS 0683212** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Ruhuwiko. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **IR/RB/6627.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MOSHI**
**TAARIFA YA SIKU YA KUSIKILIZWA RUFAA .**

**MAHAKAMA YA WILAYA MOSHI SHAURI LA RUFAA MISC.CIVIL .APPLICATION 7/2019**

**MRUFANI DAVID MATHEW NGOWO**

**DHIDI YA**

**MRUFANIWA JULIUS MWAMLIMA**

**Kwa JULIUS MWAMLIMA**
**LONGUO (B) - MOSHI**
**C/O MWENYEKITI KITONGOJI .**

Fahamu kwamba tarehe 9 mwezi 5 mwaka 2019 saa 2:30 asubuhi siku ya ALHAMISI itasikilizwa/itatajwa rufaa yako katika Mahakama ya Wilaya MOSHI imetolewa leo tarehe 25 Mwezi 4 Mwaka 2019

115211502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;102/2019**

**Ombi la PUDENSIANA JEREMIAH Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GOODLUCK HARRY EDORE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 24/04/2019.

XXXXXXX


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MADRID SASA YAMGEUGIA VAN DE BEEK




**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Ajax, Donny van de Beek, anaangaliwa kama mpango B kwa Real Madrid kipindi cha majira ya joto kama wakishindwa kumsajili nyota wa Manchester United, Paul Pogba.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 21 alifunga bao la ushindi wakati Ajax wakiibuka na ushindi kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Tottenham.

Akiwa amefunga mabao 16 na kutoa pasi za mwisho 11 kwenye mashindano yote akiwa anaichezea Ajax msimu huu, huku Van de Beek akitajwa kuwa mmoja wa nyota wenye majariwa mazuri zaidi Ulaya.

Na kwa mujibu wa gazeti la Marca, Real inamtolea macho kiungo huyo kwa ajili ya kukijenga kikosi hicho chini ya kocha mpya.

Awali Real iliikuwa inamwinda kiungo wa Manchester United, Pogba, lakini mshahara wa Mfaransa huyo unaonekana kuwa ni kikwazo kwake kuweza kutua hapo kwenye dimba la Bernabeu.

Na Van de beek anaweza kuwa mbadala wake na kwa umri wake anaweza kuwa suluhisho katika kikosi hicho cha Madrid.

Marca limeripoti kwamba anaweza kuwagharimu Real Madrid kiasi cha euro milioni 60.

Frenkie de Jong tayari ameshasajiliwa na Barcelona na patina wake, Matthijs de Ligt anaweza kumfuata.

Klabu ya Paris Saint-Germain pia imekuwa ikihusishwa na mpango wa kumtaka Van de Beek.

# Solskjaer: Tuna nafasi Ulaya

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Meneja wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amefunguka mengi kuelekea mchezo wake wa Ligi Kuu England dhidi ya Huddersfield wikiendi hii na mengi kuhusu kikosi chake cha Mashetani Wekundu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Solskjaer amesema wanaweza kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kwa sababu wana nafasi hiyo.

"Ungependa kushangaa jinsi wakala wengi wamesema kuwa wateja wao wangependa kuwa sehemu ya Manchester United katika siku zijazo.

"Hiyo ni kiu tu ya mchezaji wa Manchester United kwa sababu wanajua na uwezekano hapa na ukubwa wa klabu ambayo tutaweza kurudi siku zijazo.

"Ndio, tuna wakati mgumu kwa sasa. Tumekuwa na misimu michache ambayo hatujafikia viwango tunayotarajia lakini hiyo ni juu yangu na hadi klabu ili kuibadilisha haraka iwezekanavyo.

"Ikiwa utakuwa ni msimu bila Ligi ya Mabingwa, ni nani anayejua? Lakini wachezaji bado wanapenda kuja Manchester United na utaweza kushangazwa na majina tunayoulizwa."

"Nitakuwa msemaji wa mwisho wa kusema kama wachezaji wanaingia au kwenda nje," Solskjaer alisema.

"Tuna mikutano ya mara kwa mara. Ninafurahia njia inavyoenda.

"Tunatakiwa kusaini wachezaji 250! Unaandika juu ya wachezaji wote ambao tunapaswa kuingia lakini tunatumaini tunaweza kupata wachezaji ambao haujaandika pia."

Licha ya makosa mabaya dhidi ya Chelsea, David de Gea atakaa katika nafasi yake kwa lango siku ya safari ya Jumapili ya Huddersfield, ambayo huku Sergio Romero akiwa na matatizo ya magoti.





# *Mourinho awatolea uvivu Neville, Scholes*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ameibuka na kuwashambulia nyota wa zamani wa Manchester United, Gary Neville na Paul Scholes kwa kushindwa kupata mafanikio kwenye kazi ya ukocha.

Neville alidumu kwa kipindi kifupi kama kocha wa Valencia mwaka 2016 na Scholes hakudumu kabisa kwenye kazi hiyo wakati alipochukua mikoba ya kuinoa Oldham mapema mwaka huu.

Wawili hao walikuwa wakimshutumu zaidi Mourinho raia wa Ureno wakati wa kipindi chake pale United na sasa Mourinho ameamua kuwatolea uvivu.

Katika mahojiano yake na RT Sport, alisema: "Wanajua kuzungumza wakiwa kwenye televisheni, lakini walipopewa nafasi ya ukocha wakashindwa, inashangaza kwa kweli.

"Waliondoka kwenye klabu na baada ya miezi miwili wakaambiwa warudi nyumbani, ni kwa sababu walishindwa kupata mafanikio kama sisi wengine tulivyoweza."

Mourinho aliongeza: "Kuna sehemu moja ya uongozi, kuna watu nafikiri huwa wanasahau kuzungumza kwenye televisheni ni rahisi kuliko kuwa kwenye benchi la timu."

HABARI MICHEZO




# XAVI ATANGAZA KUSTAAFU SOKA

**BARCELONA,** Hispania

GWIJI wa zamani wa Barcelona na Hispania, Xavi Hernandez, hatimaye ametangaza rasmi atastaafu soka baada ya kucheza kwa muda wa miaka 21.

Mkongwe huyo wa Hispania, ambaye anacheza soka nchini Qatar katika Klabu ya Al Sadd, alithibitisha kwenye barua yake Alhamisi na kusema kuwa huu ni msimu wake wa mwisho kucheza soka.

"Imekuwa nafasi nzuri zaidi kwangu kucheza hadi katika umri wa miaka 39 na nitamaliza kipindi changu cha kucheza msimu huu kwa kushinda Kombe la Amir na kufuzu Ligi ya Mabingwa ya Asia.

"Huu ni msimu wangu wa mwisho kama mchezaji, kwa uhakika nataka kuona majaliwa yangu ya baadae na kuwa kocha," amesema Xavi, ambaye alijiunga na kikosi cha timu ya wakubwa ya Barca katika msimu wa 1998-99.

Zao hilo la akademi ya Barcelona aliiongoza Klabu hiyo yenye maskani yake Katalunya kutwaa mataji nane ya La Liga na manne ya ligi ya mabingwa Ulaya.

Ameshinda jumla ya mataji 31 katika ngazi ya klabu na timu ya taifa.

Ameichezea jumla ya mechi 113 timu ya taifa ya Hispania na alikuwa na mchango mkubwa kwa kikosi cha Hispania kilipotwaa ubingwa wa Kombe la Dunia mwaka 2010 pamoja na ubingwa wa Euro 2008 na Euro 2012.

Alitangaza kustaafu kuichezea timu ya taifa ya Hispania mwaka 2014.

# *Wenger atema nyongo kwa Virgil van Dijk*




**LONDON,** England

ARSENE Wenger amedai kwamba, Virgil van Dijk ndiyo aliyesababisha bao la kwanza la Barcelona kwenye dimba la Nou Camp Jumatano usiku.

Liverpool ilifungwa mabao 3-0 kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha huyo wa zamani wa Arsenal amemnyooshea kidole mchezaji huyo bora wa mwaka wa Ligi Kuu England baada ya kumruhusu, Luis Suarez kumpita kirahisi na kufunga bao kipindi cha kwanza.

"Wakati unapocheza na timu kama Barcelona, unatakiwa kuwa makini mno, lakini ni wazi kwamba Van Dijk alijisahau," amesema Wenger aliuamba mtandao wa beINsports.

"Uliona goli lilivyo, walipata nafasi moja na wakaitumia vizuri na wakafunga bao kirahisi tu."

"Van Dijk ndiye aliyebaki nyuma kama mlinzi wa wote, lakini akashindwa kumwona Suarez na akafunga kirahisi.

"Beki wa kati anatakiwa kuwa wa mwisho kuhakikisha mipira yote ya hatari inaondoka langoni mwake, lakini yeye aliacha.

"Tangu mwanzo wa mchezo, hakuonekana kuwa makini na alishindwa kuzuia kwa haraka."

# Man United kumlipa Sanchez aondoke

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inajiandaa kumlipa nusu ya mshahara wa mwezi, Alexis Sanchez kiasi cha pauni milioni 26 ili kuwezesha uhamisho wake kipindi cha majira ya joto.

Maamuzi ya mwisho ya mshambuliaji huyo wa Chile yanabakia kuwa mikononi mwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer, lakini United ipo tayari kumwachia mshambuliaji huyo.

Maafisa wa United wanajua kwamba mshahara wa Sanchez wa pauni 500,000 kwa wiki pamoja na bonasi utakuwa kizuizi.

Hivyo inaeleweka kwamba, sasa wanataka kumlipa asilimia 50 ya mshahara wake nyota huyo wa zamani wa Arsenal kama klabu nyingine itakuwa tayari kumchukua.

United inataka kumuuza Sanchez kwenda klabu nyingine baada ya nyota huyo kushinwa kung'ara tangu atue hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Sanchez tangu atue hapo Old Trafford, ameshindwa kuonyesha cheche zake kama alivyokuwa kwenye timu yake ya zamani.





# DO A SOKA MAGA A ULAYA

# MADRID, HAZARD MAMBO YAMEIVA

## ●●● Inaelezwa tayari vigogo hao wa Hispania wanasubiri muda kumtangaza...

**MADRID,** Hispania

MCHEZAJI nyota wa Chelsea, Eden Hazard (28), tayari 'ameshafikia makubaliano' ya vipengele vya maslahi atakavyopata akihamia Real Madrid katika kipindi cha majira ya joto imeelezwa.

**Klabu hiyo inatarajia kutoa taarifa rasmi za kukamilika kwa mchakato wa usajili wa Hazard ifikapo Mei 12 mwaka huu, isipokuwa kama Blues itafanikiwa kutinga hatua ya fainali ya Ligi ya Europa.**

Kiungo mchezeshaji huyo raia wa Ubelgiji alianza kuhusishwa na tetesi za kujiunga na vigogo hao wa Hispania kwa kwa miezi kadhaa iliyopita na hatimaye amekaribia mlango wa kuondoka Stamford Bridge.

Zinedine Zidane amerejea katika madaraka yake kwa nguvu na anajipanga kukiimarisha kikosi hicho cha Bernabeu na kumsajili Hazard, mchezaji ambaye aliingia akitokea benchi katika mchezo wa kwanza wa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa ambayo walitoka sare dhidi ya Frankfurt katika mchezo uliochezwa juzi usiku.

Hata hivyo, Gazeti la Marca la Hispania limeandika kuwa tayari mchakato wa usajili huo umeshakamilika lakini Real inahofia kumtangaza sasa kwa sababu haitaki kuivuruga Chelsea mpaka pale mwisho wa msimu utakapofika.

The Blues wako katikati katika safari ya kuwania kusonga mbele katika michuano hiyo na vile vile wako kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kumaliza kwenye nafasi nne za juu katika Ligi Kuu England.

Taarifa zaidi zinasema kuwa Madrid wanahofia kutangaza mapema kwa usajili wa mchezaji wao huyo bora kunaweza kuchangia kuchusha kiwango cha Chelsea baada ya mazungumzo kati ya pande hizo mbili kufanyika kwa siri.

Awali ilipanga kumtangaza mchezaji huyo ifikapo Mei 12 mwaka huu, baada ya mechi za raundi ya mwisho za Ligi Kuu England, lakini ikaamua huenda wakachelewa kufanya hivyo kama Chelsea itatinga hatua ya fainali ya michuano ya Ligi ya Europa.

Real pia imejipanga kusubiri kumalizika kwa msimu wa La Liga kwa kutangaza nyota wake wote wapya ambao imewasajili, huku ikizingatia fainali za Ligi ya Europa zimepangwa kuchezwa ifikapo Mei 29.

Marca liliandika kuwa, tayari Hazard ameshakubaliana maslahi binafsi, baada ya ada ya uhamisho kufikiwa pia. Chelsea bado itamuuza nyota huyo kwa dau la pauni milioni 120, ingawa Mbelgiji huyo mwenye umri wa miaka 28 amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

## ZISIKUPITE

### SANCHEZ HAKIJAELEWEKA

MANCHESTER United imesema iko tayari kumlipa nusu ya mshahara mshambuliaji wa Chile, Alexis Sanchez ambao ni pauni milioni 26 kama Kocha, Ole Gunnar Solskjaer ataamua kuachana na nyota huyo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mail)***

### MATA MAMBO BADO

MANCHESTER United wamempa ofa ya mwisho ya mwaka mmoja kiungo wao, Juan Mata, na inaamini kuwa Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 31 atakubali kubakia Old Trafford. ***(Manchester Evening News)***

### SESSEGNON SAFARI IMEIVA

NYOTA wa Fulham anayetumia mguu wa kushoto, Ryan Sessegnon (18), anajiandaa kujiunga na klabu ya Tottenham katika kipindi cha majira ya joto***( Mail)***

### WAN-BISSAKA AIKATAA UTD

BEKI wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka (21), amesisitiza kuwa ataendelea kubaki katika klabu hiyo katika msimu ujao licha ya kuwapo na tetesi za kutakiwa na Manchester United. ***(London Evening Standard)***

### DANILO KUTUA INTER

BEKI wa Timu ya Taifa ya Brazil na Manchester City, Danilo (27), amekubali kusaini mkataba wa miaka "minne hadi mitano" wa kutua Inter Milan ambao kwa mwaka una thamani ya Euro milioni 3.5. ***(Gazetta dello Sport, via Manchester Evening News)***

### LIGT NJIA PANDA

BEKI wa Ajax na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Matthijs de Ligt, amesema bado "anavutiwa" kujiunga na klabu nyingine licha ya kuwapo na mazungumzo ya kujiunga na Barcelona katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### OTAMENDI ANUKIA ATLETICO

MABOSI wa Atletico Madrid, wameanza mazungumzo na Manchester City kwa ajili ya kumsajili beki wake, Nicolas Otamendi ambaye ana umri wa miaka 31 na ni raia wa Argentina. ***(AS)***

### UNITED, JUVE VITANI

MANCHESTER United inachuana na Juventus katika vita vya kuwania saini ya beki wa Benfica na Timu ya Taifa ya Ureno, Ruben Dias ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Record, via Manchester Evening News)***

### DJENE ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imemtaja beki wa Getafe, Djene kuwa mmoja wa wachezaji inaowawinda katika dirisha la usajili la majira ya joto. (Marca, via Mirror)

### GOMES AGOMBEWA EPL

KOCHA Silva bado anaamini Everton itafanikiwa kumsajili kiungo wa Barcelona, Andre Gomes (25), kwa kumpa mkataba wa kudumu. Tottenham pia inatajwa kumwania nyota huyo ambaye thamani yake ni pauni milioni 30. ***(Times - subscription required)***

### KENT KUIKACHA LIVERPOOL

WINGA wa Liverpool, Ryan Kent (22), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Rangers, amethibitisha kuwa yuko tayari kuondoka Anfield, kwa sababu anastahili kupata mkataba wa kudumu. ***(Express)***



Makocha wa soka kutoka sehemu mbalimbali nchini, wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mafunzo ya mchezo huo yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Southampton ya England chini ya udhamini wa Kampuni ya SportPesa Tanzania. **PICHA: SPORTPESA**

## Sportpesa yawafunda makocha Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

MAKOCHA wa soka nchini ambao wamepata mafunzo maalum kutoka kwa wakufunzi wa timu ya Southampton kutoka England chini ya udhamini wa Kampuni ya SportPesa Tanzania wametakiwa kuyatumia mafunzo hayo kuendeleza mchezo huo hapa nchini.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, wakati wa ufungaji wa kozi hiyo ambayo ilisimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Tarimba alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa maendeleo ya soka na SportPesa Tanzania inajivunia kuwa wadau katika sekta ya michezo ambayo wanaitumia kama ushiriki wao katika masuala ya jamii.

Alisema kuwa tangu SportPesa Tanzania ianze shughuli zake hapa nchini, imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha sekta ya michezo inapata maendeleo makubwa na kujihusisha katika shughuli mbalimbali.

"Tunaomba makocha waliopata mafunzo haya kuyatumia kwa ajili ya maendeleo ya mpira nchini. Ni bahati kubwa kupata mafunzo haya ambayo yamefundishwa na makocha wenye ujuzi wa kisasa. Ni wakati wa makocha kubadilika na kwenda na wakati ili kuinua kiwango cha soka hapa nchini," alisema Tarimba.

Alisema kuwa walifanya mafunzo kwa wachezaji chipukizi wakati wa ziara ya Everton nchini na mchezaji nyota wa zamani wa klabu hiyo, Leon Osman. Mkurugenzi wa Ufundi wa TFF, Ammy Ninje mbali ya kuipongeza kampuni ya SportPesa Tanzania, amesema kuwa mafunzo hayo yamewanuifaisha makocha hao waliopata bahati ya kuhudhuria.

# WAGOMBEA UONGOZI YANGA WAENDELEA KUJINADI JIJINI

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti katika Uchaguzi Mkuu wa Yanga, Magege Chota, amesema kuwa endapo atafanikiwa kuingia madarakani atahakikisha klabu hiyo inafanya mabadiliko katika mfumo wa uendeshwaji.

**Chota ambaye alikuja katika ofisi za gazeti hili jana, alisema kuwa anahitaji kuona ndoto za kuiendesha Yanga kisasa zinafanikiwa na klabu yao inakuwa moja ya klabu tajiri hapa barani Afrika na yenye kutoa ushindani katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.**

Mgombea huyo alisema pia akifanikiwa kupata ridhaa atahakikisha anakiboresha kituo cha kukuza vipaji kilichoko klabuni hapo ili kizalishe wachezaji watakaoichezea Yanga na vile vile kuwauza kwa timu nyingine na kuipatia timu yao kipato.

"Nitahakikisha tunafanya mabadiliko katika uendeshaji, tunahamia katika mfumo mpya, tunajiendesha kisasa na kuwa taasisi imara inayojitegemea kiuchumi," alisema Chota ambaye ana kadi namba 001471 na ni mwanachama wa Tawi la Yanga Facebook lililoko Tabata jijini Dar es Salaam.

Alisema pia ataimarisha umoja ndani ya klabu hiyo na kwake anaamini makundi hayana nafasi katika kuipa maendeleo klabu yao.

Naye Fredrick Mwakalebela alisema kuwa amepanga kuanza na mambo matatu mara baada ya kufanikiwa kushinda katika nafasi hiyo.

Mwakalebela alisema baada ya kuingia madarakani atatumia nafasi yake ya uongozi kwa ajili ya kuunda mfumo bora wa uwekezaji na uendeleshaji wa klabu hiyo kwa kuwashawishi wadhamini kuingia kuwekeza klabuni hapo.

Aliongeza kuwa atawashawishi viongozi wenzake kujenga Uwanja wa Kaunda uliokuwapo Makao Makuu ya klabu hiyo utakaotumika kwa ajili ya mazoezi ili kuepuka gharama zinazotumika katika kukodisha uwanja wa mazoezi.

" Pia nikiingia madarakani nitaliboresha benchi la ufundi lililokuwapo chini ya Mwinyi Zahera, kwa kufanya usajili wa kimataifa na kisasa kwa wachezaji wenye uwezo na uzoefu wa kupambana katika Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa," alisema Mwakalebela, Katibu Mkuu wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Alisema pia ataiboresha miundombinu ya klabu hiyo ikiwamo majengo na Uwanja wa Kaunda na kupanga kujenga mkubwa wa kisasa utakaokuwa na hosteli za wachezaji.

Yanga inatarajia kufanya uchaguzi wake Jumapili kwenye Ukumbi wa Bwalo la Maafisa wa Polisi Oysterbay jijini.

# *Malindi FC, JKU mguu mmoja CAF*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Malindi na Maafande wa JKU ambazo zote zinashiriki Ligi Kuu Zanzibar zinatarajiwa kukutaka katika mchezo wa fainali wa mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani hapa.

Malindi ilitinga hatua hiyo baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 katika mchezo wa nusu fainali dhidi ya Kipanga uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Amaan, shukrani bao pekee lililofungwa na mshambuliaji, Ali Juma dakika 32.

Kipanga ambayo ilicheza punguфu baada ya mchezaji wake, Taalim Hamad kuonyeshwa kadi nyekundu baada ya kumchezea faulo nyota wa Malindi, Ibrahim Novat dakika ya 10 ilionyesha kupambana lakini walishindwa kupata bao la kusawazisha hadi mwisho wa mchezo huo.

Kwa upande wa JKU, wao walifanikiwa kusonga mbele katika mashindano hayo ambayo bingwa wake atapata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika waliwafunga Maafande wenzao wa KVZ mabao 3-0 katika mechi iliyochezwa mapema mchana juzi kwenye Uwanja wa Amaan.

Mshambuliaji wa JKU, Shehuu Mgaji alifunga hat-trick katika mchezo huo ambapo goli la kwanza lilifungwa dakika ya 56, la pili dakika ya 65 na la tatu lilikuwa ni dakika ya 73.

Kocha wa Malindi, Salehe Machupa, alisema anaamini kuwa timu yake ina uwezo wa kunyakua ubingwa wa michuano hiyo licha ya kukabiliwa na wachezaji majeruhi 13.

"Ninajipa asilimia kubwa ya kunyakuwa ubingwa huu wa FA, licha ya kukabiliwa na majeruhi wengi lakini matumaini yangu hayafutiki kuhusu hili, kikosi chetu kitashuka dimbani na wachezaji hawa ambao wameipeleka timu hatua ya fainali na tutaangalia kati ya hawa majeruhi ambao wataweza kucheza basi tutawachezesha, ikishindikana tutacheza na kikosi hiki kilichocheza leo (juzi), Machupa alisema.

Michezo

Jumamosi Mei 4, 2019

Nipashe



Madrid, Hazard mambo yameiva

HABARI UK.30



Mshambuliaji wa Arsenal, Alexandre Lacazette (kulia), akifunga bao la kusawazisha kwa timu yake katika mechi ya kwanza ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Valencia iliyochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Emirates jijini London. Arsenal ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# Igangula kutimiza ndoto za Dk. Mengi

## Ajiandaa pia "kuwashughulikia" wote waliokula mali za Yanga endapo atachaguliwa...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wanachama wa Yanga wanatarajia kushiriki kuchagua viongozi watakaowaongoza kwa muda wa miaka minne ijayo, mgombea wa nafasi ya uenyekiti, Mbaraka Igangula, amesema kuwa atahakikisha anatimiza ndoto zilizoanzishwa na Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi.

Yanga ambayo inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na pointi 74, wanatarajia kufanya uchaguzi mkuu kesho kwenye Ukumbi wa Bwalo la Maafisa wa Polisi, Oysterbay jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Igangula, alisema kuwa anaamini mabadiliko ya mfumo ndiyo suluhisho namba moja ambalo litaipa maende leo klabu yao ambayo inahitaji kujiendesha kisasa kama zilizo klabu nyingine kongwe ndani na nje ya bara la Afrika.**

Igangula alisema pia iwapo atachaguliwa kuwa mwenyekiti mpya atawashughulikia viongozi waliopita ambao waliocheza "rafu" ndani ya Yanga kama alivyofanya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

"Kumeingia mdudu ndani ya Yanga, watu wanaendesha maisha yao kwa kuibia klabu yetu, kwa sasa wanapambana ili kumwingiza madarakani mgombea ambaye atalinda uovu wao na kuwafanya waendelee kuiibia Yanga, nikiingia madarakani nitawasafisha wote hao, sitamchekea adui yeyote wa maendeleo ya Yanga," alisema Igangula jana alipokuwa anajinadi kwa wanachama wa klabu hiyo katika maeneo ya Kawe na Tabata jijini Dar es Salaam.

Makamu huyo mwenyekiti wa zamani wa Yanga alisema kuwa kwa kipindi ambacho Yanga imekuwa haina uongozi, kuna wanachama wachache ambao hawakuwa waadilifu walitumia nafasi hiyo vibaya kwa kusaini mikataba ambayo haikuwa na maslahi kwa klabu hiyo.

Mgombea huyo aliongeza kuwa anataka kuona kila kitu ndani ya klabu hiyo kinaendeshwa kisasa na uwazi huku ushindi kwa timu yao kwa kila mchezo watakaochezea ukiwa ni lazima.

"Utashangaa kuona watu wasiovuja jasho wanatumia fedha nyingi, wanajilipa posho na kujipangia matumizi makubwa badala ya wachezaji wetu ambao ndio wavuja jasho," Igangula alisema hayo alipokuwa Tabata.

Alisema pia atahakikisha anarejesha amani, umoja na mshikamano ndani ya klabu hiyo kama ilivyokuwapo miaka ya nyuma.

"Tumepoteza utamaduni wa Wana-Yanga, haupo tena kutokana na klabu kukosa viongozi waadilifu, kunahitajika mabadiliko chanya ili wanachama warejeshe imani kwa uongozi na klabu kwa ujumla," Igangula alisema.

Wakati huo huo, Elias Mwanjala, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mbeya (MREFA) na alikuwa anagombea nafasi ya Uenyekiti katika uchaguzi huo alitangaza kujitoa katika kinyang'anyiro hicho jana asubuhi.

Mbali na Igangula, wagombea wengine waliobakia katika nafasi hiyo ya juu ni pamoja na Jonas Tiboroha, Dk. Mshindo Msolla na Lucas Mashauri.

# Kagere, Mkude watetema Mbeya

**Na Isaac Kijoti,** MBEYA

KWA mara nyingine tena straika Mnyarwanda Meddie Kagere, amewanyamazisha mashabiki wa Mbeya City baada ya kufunga bao la ushindi wakati Simba ikishinda magoli 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini hapa jana.

Ikumbukwe timu hizo zilipokutana mzunguko wa kwanza katika Uwanja wa Taifa Agosti 27, mwaka jana, Simba ilishinda mabao 2-0 mabao yote yakifungwa na Kagere.

Katika mechi hiyo ambayo mabao yote ya Simba yalipatikana kipindi cha pili kwa kichwa, bao la kwanza kwa Simba lilifungwa na kiungo, Jonas Mkude likiwa ni lakusawazisha lile la kipindi cha kwanza lililofungwa na Iddi Selemani 'Naddo'.

Kwa matokeo hayo, Simba sasa imefikisha pointi 75, tano nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Yanga ambao jana walishinda 2-1 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam huo ukiwa ni mchezo wao wa 34 tofauti na watani zao walioshuka dimbani mara 29 hadi sasa.

Aidha, kwa bao hilo Kagere sasa anakaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao 17 moja mbele ya Salim Aiyee wa Mwadui FC na Heritier Makambo wa Yanga. Katika kipindi cha kwanza Mbeya City ilitawala zaidi mchezo huku mabeki wa Simba wakionekana kukatika mara kwa mara.

Dakika ya 11 kama washambuliaji wa Simba wangekuwa makini kuitendea haki krosi ya wingi wa kulia kutoka kwa Rashid Juma mambo yangeweza kuiharibikia City wakati wenyeji Mbeya City ingeweza kupata bao mapema dakika ya 17 lakini kipa, Deogratius Munishi 'Dida' alikuwa makini kuokoa shuti la Mohamed Samatta lililozaa kona. Mbeya City iliendelea kufanya mashambulizi mara kwa mara langoni mwa Simba na katika dakika ya 23 Nado aliwachambua mabeki wa Simba na kuandika bao la kwanza.

Lakini hilo halikuwakatisha tamaa kwani dakika ya 66 Mkude aliisawazishia Simba kwa kichwa akiunganisha mpira wa faulo ndogo iliyopigwa na Nicholas Gyan na dakika 81, Kagere aliiandikia Simba bao la pili kwa kichwa akiutendea haki mpira wa faulo ndogo uliopigwa na Mohamed Hussein 'Zimbwe Junior'.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >